# CONSTITUTION OF KENYA REVIEW COMMISSION

# (CKRC)

## VERBATIM REPORT OF

## CONSTITUTIONAL HEARING, SABOTI CONSTITUENCY AT SABOTI SECONDARY SCHOOL

## ON

**CONSTITUTIONAL HEARING, \SABOTI CONSTITUENCY AT SABOTI SECONDARY SCHOOL ON JUNE, 28TH, 2002**

**Present:**

Com. Maranga Charles
Com. Dr. Mosonik Arap Korir

**Secretariat Staff In Attendance:**

Hassan Mohammed – Programme Officer
Anne Cherono – Assistant Programme Officer
Suzanne Mutile – Verbatim Recorder

Pastor Patterson Kea started the meeting with a Prayer at 10.10 a.m. with Commissioner Maranga in the chair.

**Pastor Patterson:** Na tuombe,

Mungu Baba, Mungu Mwana na Mungu Roho na Mungu Roho Mtakatifu, Mungu uishiye milele, Mungu wa Abrahamu, Mungu wa Isaka na Mungu wa Yakobo, tunakushukuru Baba kwa wema wako, kwa uongozi wako, kwa baraka zako na hata baraka ya uhai ambayo umetupa siku hii ya leo, na kwa siku hii umeandaa kwa ajili ya katiba ya nchi yetu. Tunakuomba basi Baba wetu utumpe ushirika njema uongoze mwenyekiti, uwe Mwenyekiti wewe mwenyewe ukiongoza yeye, ukiwaongoza wanaoandika, utumpe mawazo ya kuwaza, mawazo njema na yenye baraka. Utumpe ufahamu njema tunapoongea na kila mnenaji Baba wetu wa mbinguni anene kutoka kwako ili mwisho wa mkutano huu uwe wenye baraka na kuwa baraka katika nchi yetu ya Kenya. Bariki kiongozi wetu wa taifa, Daniel arap Moi, anapoendelea kutuongoza. Tunaomba hayo tukiamini katika jina la Yesu Kristo aliye Mwokozi wetu, Amen.

**Wote:** Amen.

**Speaker:** Aah, Bwana Commissioners, mumekaribishwa hapa Saboti Secondary School na wananchi wa Saboti Constituency ili tuweze kutoa maoni ya kutengeneza katiba. Sasa Bwana Commissioners nataka niwaoneshe viongozi wa Constituency Constitutional Committee. Nitaanza hapo, na Bwana Joseph Khaoya simama wakuone, huyo ni member wa Constitutional Committee. Again, Mrs Jimshaw ni member wa Constitutional Committee ya Saboti, Mrs Nambane ni member wa

Constitutional Committee, Mr.Kibiswo ni member wa Constitutional Committee kutoka Cherengani, Miss Sarah Kogo ni member wa Constitutional Committee tena kutoka Cherengani, Mr. Chebii naye ni member wa Committee kutoka Cherengani, wamekuja ili watusaidie kazi.

Eeh, upande karibu na Commissioners tuna headmaster wa shule hii na ningetaka tu kwa ufupi aje hapa atukaribishe kwake.

**Headmaster:** Okay. Commissioners wa Constitution Review Commission position, eeh, Wananchi wa Saboti Division ningependa kuchukua fursa hii kuwakaribisha hapa pengine nitasema tu kuwa wanafunzi wangependa kuja lakini tutapewa nafasi baadaye. Wengi wenu ni wazazi, pengine wanaume kama mna pande ya pahali ya haja, wanaume mtaenda pande ya chini, tuko na vifaa huko chini hao wanafunzi ni vile mtatumia tu halafu wamama wataenda pande ile karibu kwa hostel dormitory ya wasichana kwa saa ya haja. Pengine msiulize baadaye mtaenda wapi. Wamama mtaenda pande ile mwisho, wanaume tuna pande ya kujisaidia upande ya chini huko. Halafu officers wa Commission tuna pahali ya waalimu watatumia pande ile.

Ningependa tu kukaribisha nyinyi hii ni siku yenu, sitaki kuchukua nafasi nyingi, mnakaribishwa sana. Asanteni sana.

**Speaker:** Okay, asante sana. Wakati unaitwa, utakuja hapa ukalie kiti na utatoa maoni yako hapa. Sasa Commissioners, Bwana Khaoya ndiye anatakiwa awe akisaidiana nanyi mkiwa na shida mnamuuliza ndio kazi inaendelea vizuri.

**Bwana Khaoya:** Yangu ni kukaribisha ma-Commissioners na tuko na majivuno vile mumepata nafasi kuja hapa by the slopes of Mt. Elgon. Ni mbali kidogo kutoka Nairobi na sitaki wachosha. Hapa vile watu walikuwa wameingia kuregister in that book, register vile mtu aliingia na tungependa kama tungefuata hiyo orodha ili tusije tukawa na marejeo mengine. Kwa hivyo narudisha hii sasa kwa mkubwa wetu leo Bwana Maranga, hatua hii naweka mbele yako utuendeshe tutoe maneno yetu. Asante.

**Com. Maranga:** Basi, asanteni. Kwanza kabisa mimi nataka kuwakaribisha na mimi nataka kutangaza hii sasa ni mkutano wa Tume ya Kurekebisha Katiba na ile sheria yoyote ambayo inahusika na hiyo Tume ya Kurekebisha Katiba. Kwa hivyo kuanzia saa hii hadi mwisho, wakati tutangaza mwisho wa kipindi huu ni mkutano wa Tume ya Kurekebisha Katiba.

Aah, kitu cha kwanza kabisa, sisi kama Wanatume kwanza kabisa ningetaka kuwajulisha ni akina nani tuko nao ili tuweze tukatoa masharti fulani ili tuweze tukajua tunatoa maoni yetu namna gani. Kwanza kabisa nataka kusema ya kuwa tuko na Commissioners watatu lakini kwa leo kuna mmoja pengine hawezi akafika kwa sababu ya sababu ambazo haziwezi kuepukika. Na kwanza kabisa tuko na Commissioner Dr.Mosonik arap Korir. Pengine awasalimie.

**Com. Dr. Mosonik arap Korir:** Hamjambo wananchi.

**Com. Maranga:** Kuna Commissioner mwingine ambaye tunamtarajia kwa sababu alikuwa na hitilafu ya gari ambaye anaitwa

Com. Abida Ali-Aroni ambaye ni makamu wa mwenyekiti wa Tume ya Kurekebisha Katiba lakini ako njiani, asipofika sio mbaya sana tuko hapa. Na huyo ndiye Commissioner wa pili. Na mimi mwenyewe naitwa Dr. Charles Maranga Bagwasi, vile vile ni Commissioner na leo mimi ndio nitakuwa mwenyekiti wa kikao cha leo. Kwa hivyo, nasema asanteni.

Vile vile tuko na wale ambao tunaita watu ambao wanatusaidia kutoka Tume ya Kurekebisha Katiba. Tuko na Programme Officer wetu ambaye anaitwa Hassan Mohammed, Mohammed waonyeshe mkono wako. Huyu ndiye anasimamia Secretariat Staff hapa. Kuna vile vile anayemsaidia anaitwa Anne Cherono, Cherono mkono yako, huyo anaitwa Assistant Programme Officer. Vile vile tunaye Susan Mutile ambaye ananasa sauti zenu wakati mnaongea. Kwa hivyo, hawa ndiyo timu yetu na wakati wowote una taabu zozote, tafadhalini ona huyu tunaita Hassan Mohammed. Kama una jambo lolote la kuelezea ama nini, uelezee Mohammed. Na vile vile tuko na wazee wa nyumbani hapa ambao wale mnaita 3C's wako hapa vile vile ni part ya Tume ya Kurekebisha Katiba.

Aah, wacha niwapatie masharti kidogo. Kwanza kabisa, hiki kikao ni wazi kwa kila Mkenya na Mkenya ni mtu yoyote awe askari polisi, awe askari kanga, awe mwananchi wa kawaida, una haki ya kutoa maoni mbele ya Tume ya Kurekebisha Katiba. Sheria ambayo sisi tunatumia ina haki ya kila Mkenya kutoa hoja zake mbele ya Tume vile anavyotaka. Na kuna njia, eeh, kuna njia tatu ambazo unaweza kutoa maoni mbele ya Tume. Kwanza kabisa unaweza ukatoa maoni mbele ya Tume kwa kutoa maoni yako kwa kuongea. Sisi tunakubali hayo kwa sababu unaweza ukatoa maoni yako na unaswe na sauti. Kila kikao hiki cha Tume, sisi tunafanya kitu tunaita recording ama kunasa sauti zenu vile unavyoongea. Kwa hivyo hakuna jambo lolote ambalo linaweza likatokea. Hata ukiona Commissioner mwenzangu Dr. Mosonik arap Korir haandiki kila chochote ambacho wewe unazungumzia ni kwa sababu tunanasa maneno yako kwa tape. Na hizi zitaenda kuandikishwa tena huko Headquarters ili tuweze tukapata kamili kabisa watu wa Saboti walisema nini. Kwa mfano, kama mtu wa kwanza kabisa atakayeongea hapa anaitwa Wilson Juma Makete, Makete sasa atanaswa na sauti yake na vile anavyoongea. Sisi tutaenda kuandikisha huko, hii report itarudishwa hapa kwa Constituency muone Bwana Makete alisema nini. Hata kama umekohoa mahali fulani, hiyo sauti tunanasa. Tunasikiza hiyo maneno?

**Wote:** Ndio.

**Com. Maranga:** Kwa hivyo, hakuna ile kitu ambacho kitapotea. Usije ukasema kwa nini Commissioners hawaandiki, mimi naona Mosonik ananiangalia tu nikiongea ama Maranga, tunaelewana hivyo?

**Wote**: Ndio.

**Com. Maranga:** Tunanasa kila kitu. Haya, ya pili kabisa, kwa hivyo unaweza ukakuja mbele ya Tume uongee na utoe maoni yako.

Pili, inatakikana unaweza ukatoa maoni yako kwa njia ya nakala ama memorandum. Kama umeandika karatasi yoyote, memorandum sio lazima iwe imechapwa na typewriter, unaweza tu ukaandika kwa mkono utupatie hii ndio maoni yetu. Hiyo ni njia moja. Unaweza ukajiandikisha, ukafika kwa Hassan ujiandikishe utoane memorandum kama unaenda kazi yako Kitale uelekee bila kuongojea. Tunaelewana?

**Wote:** Ndio.

**Com. Maranga:** Njia ingine ya tatu ni mtu ambaye anaweza akataka kutoa maoni ameandika memorandum lakini kuna points zile za muhimu anataka kupendekeza kwetu. Na hiyo vile vile unatakiwa kufanya nini? Kupendekeza hiyo. Saa hii kuna muda sisi tutapeana, kwa yule mtu ambaye ako na memorandum tunampa muda mdogo tu ni chache kabisa ili aweze akatoa maoni. Lakini kwa leo, kwa sababu naona wananchi wengi sana wamejitokeza na hatutaki mtu yeyote awachiliwe mbali, tunataka kama unasema maoni yako uyaseme kwa ufupi kabisa na uweze ukapeana vile inatakikana.

Kwa mfano, kama ni taabu za maneno za mashamba sijui taabu za watu wa Saboti, kuongea maneno ya mashamba, ndio. Lakini pendekeza kwa Tume unataka tufanye nini? Hiyo ndiyo kazi ya muhimu. Kulalamika tu haitoshi, unalalamika na unatupa nini? Pendekezo. Unasema mimi fulani kitu kinanisumbua hapa ni maneno ya security, kama ni hiyo security tuambie unataka namna gani. Ama unasema hapa mimi vile nakaa hapa mimi naona mtu ananisumbua zaidi ni Bwana Chief. Pendekeza, unataka huyo chief asije akakusumbua siku ingine namna gani, tunaelewana? Hayo ndiyo mapendekezo tunataka kama Tume. Kwa hivyo usije ukalalamika tu bila kumpa sisi mapendekezo kwa sababu watu ni wengi na kila mtu anatakiwa kupewa nafasi. Je, nyinyi mngetaka watu wawili watatu waongee kwa niaba yenu?

**Wote:** Hapana.

**Com. Maranga:** Basi, kama hamtaki hivyo muda ambao tutampa mtu tunataka tukubaliane sasa kikatiba, tunaelewana? Tunataka tukubaliane nini? Kikatiba. Wale watu wamejiandikisha hapa kulingana na list zile tumeona hapa ni kama watu mia mbili sasa. Na kama tukimpa kila mtu dakika kumi hiyo itakuwa sijui dakika elfu mbili na hiyo hata haiwezi kuwa, na dakika elfu mbili wale watu wanajua hesabu, hiyo ni masaa mangapi? Itakuwa usiku, tena tutaenda siku ingine, hiyo haiwezekani. Si ni hivyo? Tunaelewana?

**Wote:** Ndio.

**Com. Maranga:** Kama ni dakika tano vile vile hivyo haiwezekani. Sasa mimi nasema hivi, tukubaliane. Mtu akija mbele yetu hata kama wewe uko na maoni tupeane kwa dakika tatu, tupeane kwa dakika ngapi? Tatu. Tunakubaliana? Dakika tatu, unafanya summary, unasema mimi ni fulani, mimi ni Bwana Wilson Makete maoni yangu ni hii. Na mimi kama mwenyekiti, kwa sababu tumekubaliana ni dakika tatu, mimi nina haki ya kukatisha maoni yako, tumekubaliana? Mumenikubalia nikukatishe

wakati umezidi dakika tatu?

**Wote:** Ndio.

**Com. Maranga:** Ndio watu waongee?

**Wote:** Ndio.

**Com. Maranga:** Hebu nione wale ambao tunakubaliana kwa kwa mkono. Basi, hiyo ni katiba. Hiyo tumeandika kikatiba, muda wetu ni dakika tatu kwa kila mtu. Sawa tu, dakika tatu, na utaona dakika tatu ni muhimu sana.

**Speaker:** Dakika tano basi.

**Com. Maranga:** Aa aah, tano watu wengi hawataongea na mimi najua wengine mnarudi mbalimbali, mumetoka wengine mbali sana na watu wamejiandikisha. Haya, kikatiba ingine ya pili tutafuata hii list vile mumeingia. Mimi nimempatia kama Bwana Makete ndio mtu wa kwanza, hii hakuna njia yoyote, tunaelewana? Atakayefuata yeye ni Masengeli, atayefuata yeye ni Mutasi ambaye anafuata ni Makokha, tunaelewana?

**Wote:** Ndio.

**Com. Maranga:** Kwa hivyo hiyo ndiyo list nitafuata. Kitu kingine mimi nataka niwaambie, ukikuja hapa kwa hii mashine ya kunasa sauti unaanza kwa majina yako. Sababu tunakwambia uanze kwa majina yako kamili ni kwa sababu sisi tunanasa ili wakati tunaandika report tunajua hiyo report ilitokana na Masengeli, hii report ilitokana na Makete. Kwa hivyo usije ukaaibika wakati tunasoma historia wewe uonekane ulitoa maoni si ya maana. Kwa hivyo ukija hapa toa maoni ya maana, tunaelewana?

**Wote:** Ndio.

**Com. Maranga:** Kama wewe unakuja hapa kuzungumza maneno ambayo si ya maana, ni watoto wako watakuja kusoma na wajukuu wajue ulisema nini, ama namna gani?

**Wote:** Ndio.

**Com. Maranga:** Kitu kingine, hapa hatutaji majina ya watu. Hata kama Chief, D.O, Mbunge hata awe ni nani, hutaji mtu kwa jina. Wewe unakuja hapa unasema mimi naongea ofisi ya Rais. Mimi nataka ofisi ya Rais iwe namna hii. Ukija hapa kama unaongea kuhusu ofisi ya chief, hapana taja chief ambaye anatoka location yako. Sema mimi ma-chief nataka wawe

namna hii, tunaelewana? Kama ni police, hapana taja police fulani, wewe sema maneno ya police, tunaelewana? Hiyo ni sawa sawa?

**Wote:** Sawa.

**Com. Maranga:** Kwa sababu sasa ukitaja fulani na fulani na yeye aje aseme huyu fulani ameongea namna hii, sisi sio korti leo hapa, sisi tunataka kuchukua maoni, tunaelewana?

Okay, ingine ambayo mimi nataka kuwaambia ni kuwa kama hutaki kuongea mbele ya Tume hata kama umejiandikisha hapa, tunaelewana? Kama hautaki kuongea vile vile unaweza ukaniambia Bwana Chairman maoni yangu yametolewa na fulani, sina haja ya kuongea, tunaelewana?

**Wote:** Ndio.

**Com. Maranga:** Na kwa hivyo kuna watu ambao mnaweza mkakuja hapa, mkaketi mkasikiza, msikie vile wengine wanaongea. Kwa hivyo hiyo nayo vile inafanya nini? Inakubaliwa. Mwisho kabisa, wakati umeshaongea hapa, ukishamaliza dakika yako tatu, unaenda huko kwa Bwana Hassan Mohammed kuna kitabu chetu ambacho tunasema ni official register ya Commission, unajiandikisha unaweka sahihi. Hiyo ndiyo tutaweka ndio baadaye ukitaka kusema mimi nilitoa maoni hapa Saboti Secondary School, wapi report hiyo? Wacha nione kama ulitoa, tumeelewana? Basi kuanzia sasa ni kuanza kuita watu moja kwa moja na watu tafadhalini kitu ingine mheshimu maoni ya wenzenu. Hata kama mtu anaongea vibaya kabisa, usiwe na moyo wa kusema ati ho! Eeh ni nini, kwa nini huyu anaongea namna hii? Kama mtu anasema anataka majimbo, sawa sawa, hiyo ni haki yake. Kama mwingine anasema anataka Serikali ya umoja, hiyo ni haki yake. Hata kama mwingine anasema chochote, hiyo ni haki yake. Kwa hivyo msianze kusema aah, hiyo sio mzuri, unasikiza mtu kama wewe unataka kugeuza hayo maoni yake, kuja utoe maoni yako ambayo ni kinyume ya yule mwingine. Hii ni kama debate, ni kama nini? Debate, na huwezi ukatukana mtu yeyote na mtu ambaye unapeana maoni sio hawa wamekuja kusema hapa, ni sisi wanatume, tunaelewana? Hao wengine ni wasikilizaji tu na wanakuja kutoa maoni.

Mwisho kabisa, mtu anaweza kuongea lugha yoyote. Unaweza kuongea lugha ya Kiswahili, unaweza ukaongea lugha ya kimombo, unaweza ukaongea lugha ya mama. Kama hapa lugha ya pande hii mtu anaweza akaongea kama haelewi Kiswahili na Kimombo lakini mjue ya kuwa ile dakika tatu kama unataka mtu atafsiri maneno yako, vile vile inahesabiwa, tunaelewana? Tuelewane hivyo, kama mtu unakuja hapa unataka kuongea lugha ya Saboti ama Kiluhya ama nini inatakikana sisi tufanye nini? Tafsiri. Kwa hivyo kama unaona hiyo dakika yako itaisha haraka ni vizuri na unaona Maranga ametoa saa na nimeweka mbele yangu, tumeelewana? Sasa hiyo ni kuonyesha kazi karibu kuanza.

Basi, mtu wa kwanza kabisa ……… kwa hivyo wakati unafanya registration huko, tuonyeshe kama unataka kuja kuongea ama

unakuja kukaa hapa ndani kama observer yaani mtu ambaye anakaa kwa mkutano asikize wengine, hakuna ubaya , inakubalika tu. Sio lazima kila mtu aongee. Pengine point ile yako mtu alikuwa anataka kuongea vile vile imeshaongewa, na kwa hivyo kumalizia tu jameni leteni mapendekezo. Watu wa Saboti kitu kitatusaidia kama Wanatume ni yale mapendekezo yenu. Kama ni elimu unaongea, usituambie maneno mingi kuhusu elimu, hata sisi ni Wana Kenya. Ongea tu kidogo unasema napendekeza hivi. Ongea hivi unapendekeza hivi, tunaelewana? Basi, Bwana Wilson Juma Makete, mtu wa kwanza, dakika tatu. Anza kwa majina yako Mzee.

**Wilson Juma Makete:** Asante sana Commission, mimi naitwa Wilson Juma Makete. Kushaandika Wilson Juma Makete? Sasa neno langu ambalo mimi nataka zungumza hapa, nataka nione maoni yangu kitu kinanisumbua ni harambee. Nataka hii Commission kama inawezekana watoe harambee. Kitu cha pili warudishe control prices, control prices sababu hii vile sisi watu ya ukulima tunaumia nayo kwa habari ya watu wengine wanafanya free. Watu kuleta vitu nje kuleta hapa na hii kama mahindi na sisi tunaumia na mahindi yetu hatuuziwi bei nzuri. Kitu cha tatu nataka President awe kwa miaka mitano ndio kitu ambacho mimi niko nacho hapa kwa roho yangu.

**Com. Maranga:** Unaambiwa urudie.

**Wilson Juma Makete:** Ndio hapo, ya ya nyuma?

**Com. Maranga:** Hiyo hiyo umesema.

**Wilson:** Ya President?

**Com. Maranga:** Hapana hiyo ya…ya President iwe miaka?

**Wilson:** Miaka mitano.

**Com. Maranga:** Okay.

**Wilson:** Ndio.
**Com. Maranga:** Thank you.

**Wilson:** Tuseme kama vile mimi nakusasema mambo ya kwanza ya kutoa harambee halafu ya pili eeh control price inarudi kwa control na hii ndio kitu ambaye itaweza saidia sisi wakati ujao. Kama wakulima tunaweza kupata aah, tunaweza kupata njia ya kuuza mahindi yetu badala ya sisi saa hii tunauza mahindi kwa gunia mia nne na mahindi inatakiwa tuuze kwa gunia elfu moja mia mbili.

**Com. Maranga:** Ya mwisho Mzee wangu.

**Wilson:** Hiyo ndio sasa ya mwisho kabisa.

**Com. Maranga:** Asante sana, nashukuru.

**Wilson:** Haya.

**Com. Maranga:** Aah, na sasa…hebu niwekee sauti kwa hii kitu. Aah na mimi nataka kukuambia ya kuwa asante kwa kutoa maoni na nakuomba uweke sahihi kitabu chetu rasmi. Asante sana, hiyo hapo. Anayefuata anaitwa Wycliffe Masengeli, Wycliffe? Keti, yule atafuata yeye ni Francis Mutasi, ako Francis Mutasi, Francis, ndio wewe?

**Francis:** Ndio mimi.

**Com. Maranga:** Basi uwe tayari tu. Mimi nataka uwe tayari, asante. Na tena kitu ingine ningewaelezea kuwa sisi kama Commissioners kama unatoa oni fulani na tunataka tujue kwa undani kidogo vile unamaanisha, tunaweza tukakuuliza swali ili tu uweze ukatufafanulia zaidi unamaanisha nini, tunaelewana?

**Wote:** Ndio.

**Com. Maranga:** Asante, endelea kwa majina kwanza.

**Wycliffe Masengeli:** Eeh, kwa majina naitwa Wycliffe Masengeli kutoka Saboti Division. Nitaanza na kuzungumzia juu ya afisi ya Rais. Naona ya kwamba mtu ambaye anataka kugombea kiti cha Urais asiwe Mbunge. Na pili tuone ya kwamba atawajibika kwa mihula miwili ya miaka mitano katika ofisi ile. Mamlaka yake ya kuwa Amiri Jeshi na kuteua afisa kama Attorney General, kuteua kama Auditor General na Mkuu wa Sheria iondolewe katika ofisi hiyo, na alindwe na sheria mpaka atakapomaliza muhula wake. Akiwa atatoka ofisini na makosa, ashtakiwe baadaye.

Naona ya kwamba Serikali iwajibike iwe ya Bunge, kiongozi awe ni Waziri Mkuu kuhusu hiyo Bunge na aajibike kwa ajili ya maswala ya kisheria. Jambo lingine nimeona ya kwamba tume zote nchini ambazo ikiwemo Tume ya Marekebisho ya Katiba iwe chini ya mamlaka ya Bunge ndiyo iwajibike kwa mambo kama hayo na marekebisho mengine.

Ninakuja katika afisi ya Mkuu wa Sheria, afisi ya Attorney General, Auditor General, Speaker au Mkuu wa Jeshi, hawa nyadhifa za ofisi hizi zote ziteuliwe na Bunge ili waajibike kwa Bunge kwa wakati wote watakuwa ofisini mwao. Na wawe na ulinzi katika afisi zao wasiwe wakitolewa bila sababu iliyo maalum.

Umilikaji wa ardhi – Naona katika nchi yetu umilikaji wa ardhi hauendi sambamba na mahitaji ya wakaaji wa mahali pale. Kuna ardhi ambayo inayomilikiwa na Serikali, kuna ardhi ambayo watu wamenunua kutoka kwa wazungu walioacha mashamba na huku tungali tunalipa ushuru, umepata title deed na unalipa ushuru. Tunataka huo ushuru ukatolewe ili kila mtu awe na kibali maalum na kumiliki shamba lake. Tunaona ya kwamba kama rasilmali ya Serikali kama mashamba, misitu, watu wanaokaa eneo hilo waajibike kwa asili mia thelathini na Serikali iwe na asilimia sabini katika hayo mambo.

Walemavu wamesahauliwa sana katika nchi yetu hii, ninaomba ya kwamba Serikali iangalie mambo yao ya elimu, mambo ya kibiashara na hata ikiwezekana wanapoteua Wabunge maalum wawe walemavu na watu wasiojiweza katika hali yao.

**Com. Maranga:** Ya mwisho.

**Wycliffe:** Naona ya kwamba uchaguzi wa Urais uwe awe na asilimia thelathini katika kura zote kwa mikoa mitano na katika uraia naona ya kwamba raia yeyote wa Kenya aishi mahali kokote anakotaka anapochagua yeye mwenyewe na sheria imlinde, imtunze mahali hapo kwa ajili ya mali yake na umilikaji wa yote aliyo nayo.

Serikali iajibike kwa ajili ya kutuondolea biashara huru. Biashara huru imeleta taabu kwa mkulima na tena Serikali iwajibike kwa mavuno ambaye tunayozalisha katika nchi ya Kenya isitolewe kutoka nchi ya ng'ambo ili ikoseshe soko ya mazao yetu. Naona ya kwamba ninapomalizia nasema ya kwamba walemavu wote nchini wapewe fursa ya kusoma bure masomo yao katika viwango vile watakavyowezekana kusoma. Mungu…

**Com. Maranga:** Okay, endelea. Thank you very much.

**Wycliffe:** Nasema ya kwamba, Mungu na awabariki Tume hii ili maoni haya yatekelezwe jinsi wananchi wanavyotaka.

**Com. Maranga:** Asante, Masengeli hiyo memorandum uweke jina lako upatiane kwa Programme Officer wetu kwa sababu hiyo ni nakala ya muhimu kwetu. Thank you very much. Mzee Mutasi halafu atafuatwa na…

**Mutasi:** (Inaudible)----

**Com. Maranga:**…amesema ile umesema, asante. Basi asante, thank you very much, Okay, thank you very much. Moses Makokha, Moses? You are next please. Atafuatwa na Rachael Sutuma, Rachael ako, Rachael? Basi baada ya…Fra, eeh Makhoha huji, Moses hataki kuongea?

**Moses:** Nitaongea.

**Com. Maranga:** Basi kuja sisi wewe ndiwe naongojea, jameni, na Rachael Sutuma, wewe ndio utafuata Moses, sawasawa? Thank you.

**Moses Makokha:** Asante sana. Kwa majina ni Moses Makokha kutoka katika Location ama Division ya Saboti katika soko la Moroki. Kwa hivyo mimi wazo langu la kwanza ama pendekezo langu katika Tume hii ni katika sehemu ya ofisi ya chief. Ni kwamba chief awe akipigwa transfer kwa sababu yeye ni mfanyi kazi wa Serikali na kama hapigwi transfer, basi pia achaguliwe na wananchi kwa baada ya kipindi cha miaka mitano.

Sehemu yangu ya pili ni kwamba sehemu ya ukulima. Vyombo vyote ama bidhaa za ukulima zisitozwe ushuru na Serikali na kwa sababu katika sehemu hii wakulima wananyanyaswa kabisa vitu kama mbolea, mbegu vinatozwa ushuru wa hali ya juu na wakati wakulima wanavuna mavuno yao pia wanapoenda kuuza katika masoko pia wanatozwa pia ushuru kwa hivyo mambo hayo yaondolewe.

Sehemu ya tatu ni kazi – Mfanyi kazi katika nchi yetu ya Kenya, idara zote za Serikali ziangaliwe kwa uangalifu kabisa ili ya kwamba wote wanaoajiriwa katika idara zote za Serikali, wawe wamewakilishwa kutoka makabila yote arobaini na mbili kutoka katika nchi yetu ya Kenya. Kwa sababu wakati mwingine ukienda katika maofisi utapata kuna kabila moja ambalo linafanya kazi hapo na ilhali katika nchi yetu ya Kenya kuna makabila mengi.

Basi katika sehemu yangu ya nne ambayo ni ya mwisho ni kwamba nazungumzia juu ya squatter. Mashamba ambayo yanapewa squatters wetu katika nchi yetu ya Kenya, Serikali yetu ifuatilie kabisa na kuhakikisha kwamba anayepewa shamba kama squatter awe ni squatter kamili kwa sababu kuna watu ambao hawana chochote kabisa, wanaishi masokoni na kuna mtu ambaye anamiliki shamba la ekari hamsini, ekari mia moja labda mwingine pia amefanikiwa na ekari kama kumi lakini wanapokaa wa-squatters unakuta amepata sehemu kila mahali amejiingiza kuwa yeye ni squatter. Na kwa hivyo squatter halisi yeye anapatikana ya kwamba hana chochote, hana mbele wala nyuma.
Na kwa hayo machache Mungu na aweze kuwabariki.
**Com. Maranga:** Aah, swali moja.

**Moses:** Asante.

**Com. Maranga:** Moses, kwa mfano, kama tuseme tuamue tupatie squatters wote shamba, eeh kwa mfano,

**Moses:** Yes.

**Com. Maranga:** inamaanisha kuwa hatutakuwa na squatters wengine baada ya kupeana squatters wako Kenya hii sasa?

**Moses:** Squatter hawakwishi,

**Com. Maranga:** Mimi nauliza, kuna njia ingine yoyote tunaweza kusaidia squatters, maybe badala ya kuwapatia mashamba. Kwa mfano, kama squatter akipatiwa acre moja, hiyo kweli itamtosheleza na familia yake kulima na kukaa na nini? Si hao watoto wake tena wataanza kuwa squatters?

**Moses:** Haimtoshelezi, kwa hivyo napendekeza ya kwamba katika sehemu hiyo napendekeza ya kwamba Serikali iwe ikiangalia watu kama hawa na wawe wakipewa marupurupu mwisho wa mwezi ikiwezekana,

**Com. Maranga:** Social Welfare?
**Moses:** Yeah,

**Com. Maranga:** Thank you very much.

**Moses:** Kwa ajili ya kuwainua.

**Com. Maranga:** Asante sana, kwenda weka sahihi huko. Haya Rachael Situma? Unaanza kwa majina yako mama. Chukua hiyo mike na uanze kuongea. Anza na majina.

**Rachael Situma:** *Lisina, ndangwa Rachel…..*

**Com. Maranga:** Okay, ngoja hebu tupate ambaye anatafsiri. Nani yule atatusaidia? Okay, thank you, he is there. Unaongea vile anaongea, usije ukatafsiri usiongezee, unaongea vile anaongea.

**Rachael:** *Lisina liase Rachel Naliaka Stiuma.*

**Translator:** Majina yake ni Rachael Naliaka Situma.

**Rachael:** *Ese nechile anano khulondekhana nende eofisi yefwe ya Chief.*

**Translator:** Amekuja hapa kwa ajili ya ofisi ya chief.

**Rachael:** *Khulondekhana nende bakhasi nibo basakhulu babwe bafwichanga.*

**Translator:** Kwa ajili ya wamama wajane,

**Rachael:** *banyolanga basakhulu babandi babeelangakho, mala nga neboola ao, benya bababukule kimikunda ekio babalekhe ao busa.*

**Translator:** wameridhiwa na wanaume wengine na wanataka kuwapokonya hiyo mali ya ardhi.

**Rachael:** *Nono liliene eli, efwe khulalolanga khuli lisiro nilio. Baleenyala bariena?*

**Translator:** Sisi tunaangalia hiyo jambo ni mzito sasa watajiwezaje?

**Rachael:** *Lundi bali ne babana benya basome.*

**Translator:** Wana watoto wanaotaka elimu.

**Rachael:** *Mala baababukula bulime.*

**Translator:** Wamewapokonya mashamba.

**Rachael:** *Balanyola bariena makao?*

**Translator:** Watapataje sasa makao?

**Rachael:** *Namwe maendeleo balanyala bariena?*

**Translator:** Watafanyaje maendeleo?

**Com. Maranga:** Unapendekeza nini?

**Rachael:** *Nenya babayete.*

**Translator:** Anapendekeza ya kwamba wasaidiwe.

**Com. Maranga:** Ongoja kidogo, anaendelea? Okay, endelea tu.

**Rachael:** *Nilio mbendelea Lundi, ese ndola ndi efwe efwe elubeka we ofisi, khuli bakasa, mala nifwe emoni ya Raisi*

*musirekere, -mu Trans Nzoia muno.*

**Translator**: Anaonelea ya kwamba yeye ni mzee wa vijiji na hao ndio macho ya Serikali katika Trans Nzoia.

**Rachael:** *Nono khukanakana khwase mbola ndi, Serikali ikhoya fwesi ikhulole emoni ne khunyolangakho sindu sititi.*

**Translator:** Anasema ya kwamba wazee wa mitaa wawe wakipata marupurupu.

**Com. Maranga:** Asante mama, lakini ngojea kidogo kuna swali kutoka kwa Commissioner mwenzangu.

**Com. Mosonik:** Mama akasema kuhusu chief, alianzia kusema chief na hakukuwa na mapendekezo.

**Rachael:** *Efwefwe nono khwichanga mu-staff yefwe khu Chief. Nono nga nekhwichanga, khwamanya khuli Harambee chilikho.*

**Translator:** Huwa wanakuja katika staff yao katika afisi ya chief na wanajua ya kwamba harambee ziko.

**Com. Maranga:** Oo ooh, kwa hivyo chief anawadai harambee?

**Rachael:** *Efwefwe nga khuchangishanga Harambee chino, nono abwene ao nio khulililа bakasa khuli andi fwesi abechanga khunyolakho sindu sititi, nio be…*

**Com. Maranga:** Okay, very good.

**Translator:** Okay, wanachangisha harambee na analia ya kwamba pia hao wapewe sehemu.

**Rachael:** *Sekhwinyala khu…*

**Translator:** Kwa maana hawajiwezi.

**Com. Maranga:** Okay, asante. Okay, jiandikishe hapo, mwambie ajiandikishe hapo. Okay, yule anayefuata sasa anaitwa Moses Supu, Moses Supu ako, Moses? Ni wewe, unataka kutoa maoni? Haya, endelea. Una dakika tatu na unaanza na majina yako.

**Moses Supu:** Aah, mimi majina yangu ni Moses Supu. Maoni yangu ya kwanza ni kwamba kabla squatters wale ambao

wanaandikwa waweze kupewa mashamba, kwanza wangekumbukwa wale walifukuzwa kutoka ndani ya forest. Kwa maana kuna watu waliotolewa ndani ya msitu miaka zilizopita lakini mpaka sasa wanakaa masokoni na kwa manyumba za wengine, hawana mahali pa kuishi. Kama ingewezekana wangeangalia majina yao kwanza wapewe mashamba ili wengine waangaliwe baadaye.

Jambo lingine la pili ni kuhusu makanisa - Katiba yetu pia ingeliruhusu wale wahubiri wadogo wadogo ambao ndio wanaanza wawe registered na wasipewe vikwazo nyingi sana wanapojiandikisha.
Na singekua na mengi zaidi hapo maana mengi yamesemwa.

**Com. Maranga:** Bwana Moses, ningekuuliza hivi, hii makanisa kidogo kidogo tunasikia wananchi wengine wanasema mengine hii makanisa kidogo kidogo imeleta vurugu nyingi sana kwa makanisa kubwa. Utasemaje kwa hayo?

**Moses:** Shida ya makanisa madogo na makubwa kuleta vurugu ni kwa sababu wale wakubwa wanaona kwamba ni hao tu wangestahili. Lakini kwa Mungu sote tuko sawa na inawezekana tuwe wahubiri kama sawa na wao.

**Com. Maranga:** Okay. Haya asante, weka sahihi Moses Supu. Anayefuata ni Councillor Nana Daniel, good, karibu Councillor. Atafuatwa na Protus Nyongesa, Nyongesa ako? Basi wewe uwe tayari wakati Councillor anamaliza, wewe ndiwe wa kwanza huko. Ngoja utafuata, thank you.

**Daniel Nana:** Mimi ni Daniel Nana, Councillor Saboti Ward. Nazungumza kuhusu upeanaji wa ardhi. Upeanaji wa ardhi uwe unasimamiwa na community ambayo inazunguka kwa area hiyo. Sioni sababu yoyote allotment kutoka juu iwe inapeanwa kama kwa ma-D.C, iwe inapeanwa watu ambao wanaweza kujimudu. Sisemi ya kwamba kila Mkenya apate shamba, lakini kama mashamba makubwa kama ya A.D.C, kama ingekuwa inatoa kazi kwa wananchi wangefaidika zaidi.

Neno lingine ambalo ningelisema kufuatana na polisi kushika wahalifu. Polisi akishahakikisha ya kwamba mtu ana hatia ya kushikwa kwa maana amefanya kosa ambalo anastahili ashikwe na afikishwe mahakamani haraka inavyowezekana. Sio kuweka kwa police cells kwa muda ambao usifae.

Nakuja upande wa kukunywa pombe - kunywa pombe tunalaani ulevi, hata pombe ya kizungu ni pombe. Lakini kama Waafrika wangepewa pahali yao kama wanamaliza kazi wapumzike ni kama Busaa na mambo mengine kwa maana hawawezi kukaa tu na pombe ya kizungu iko bei hii ya hali ya juu.

Kuhusu ulinzi – Ulinzi si nzuri sana hasa wizi wa mifugo na unajua Mkenya ukipoteza hata ng’ombe mmoja, kumpata mwingine ni ngumu.

Elimu – Elimu ingekua Serikali ingesimamia tuone ya kwamba elimu ya msingi inakuwa ya bure kuwezesha kila Mkenya apate kuelimika. Matibabu yangefanywa vivyo hivyo hivyo.

Mambo ya upeanaji wa mashamba kwa wamama – Wamama wengi wanakuwa fukara kwa sababu ma-title deeds au vyeti vya kumiliki mashamba viko kwa wazee pekee yao. Na ingekuwako vile wamama wawe na majina yao kwa title deeds ili wasiwe fukara kwa maana mambo mengi yanafanyika sasa hapa mama wengi hawana mabwana na hawana mashamba.

Ofisi ya President, Prime Minister aingie ndani. Aah, Wakenya – Wakenya wakiwa wazazi wawili, anakubaliwa kila mara moja awe Mkenya na kama mmoja ni Mkenya, apewe kitambulisho. Na Mkenya ambaye anahitimu miaka kumi na nane, apewe kitambulisho haraka inavyowezekana.

**Com. Maranga:** Ya mwisho, Councillor.

**Daniel:** Ya mwisho ni nauliza Tume iwakilishe kwa njia ya uhaki namna tunavyoendelea na kwa kuwekwa mabadiliko ili tusiwe na mahangaiko kama katiba ile iliyokwisha.

**Com. Maranga:** Basi nataka kushukuru wewe kwa maoni yako na nimeona wewe iko na memorandum kubwa kabisa, hiyo memorandum utupatie ama hiyo sio memorandum?

**Daniel:** No, memorandum nitakupatia.

**Com. Maranga:** Eeh, utatupatia na uweke sahihi, asante sana kwa maoni yako.

**Daniel:** Asante.

**Com. Maranga:** Tunashukuru, thank you. And next, Nyongesa. Aah, Mr. Nyongesa atafuatwa na Japheth Wetungu, ako? Where is Wetungu, Wetungu ako wapi? Hayuko, unataka kuongea, Japheth, wapi Japheth Wetungu, utaongea?

**Japheth:** Memorandum.

**Com. Maranga:** Basi asante. Eeh, Andrew Majune?

**Wote:** Ako.

**Com. Maranga:** Utaongea?

**Andrew:** Sawa.

**Com. Maranga**: Sawa basi uwe tayari. Endelea.

**Protus Wangila Nyongesa:** Asante sana Tume ya…

**Com. Maranga:** Chukua mike, uanze kwa majina yako.

**Protus:** Mimi naitwa Protus Wangila Nyongesa. Hapa katika mbele ya Tume nafikiri nitaripoti kisanga juu ya umasikini ambao ni ugonjwa mkubwa sana ambao umejikita eneo la Trans Nzoia kwa ujumla sawa na Ukimwi. Mimi kwanza ninavyoongea ninajihisi kwamba matajiri ambao wamemiliki mashamba ambayo yalikuwa ya wazungu wanawagandamiza Waafrika wenzao. Ya kwanza mishahara ni ya chini sana, mtu kafanyie shilingi sitini ilhali hana shamba na watoto wanaenda shule. Mishahara kwa ujumla iangaliwe katika mashirika ya Serikali na ufisadi, jambo ambalo limeleta ubaguzi, ukabila ndani yake.

Upande wa unyanyasaji nafikiri, upande wa chief ama ofisi tawala, nafikiri wengi wamesumbuliwa sana area hii kwa upande wa vinywaji kama alivyosema mwenzangu nitagusia pale. Utapata kuona kwamba maaskari wanapohusika sana sana katika maeneo ya kunasia pombe haramu ambayo imepigwa marufuku wataitisha hongo – shilingi elfu mbili. Jambo ambalo ni sawa na kupanda mchongoma kwa huyu masikini, upwete. Jambo lingine nitagusia hapa ni kuhusu ule umasikini Serikali iangalie sana, itenge maeneo ambayo wale watu masikini watapewa kulima. Sana sana nakumbuka mambo hayo yanayotendeka kule Tanzania. Mashamba ya ubwete, mtu akalima akapata yake akanunua akaenda, akawachia wengine. Asante sana.

Upande mwingine nitagusia ni wa usalama kuhusu ma-home guards wale waliokwenda shule wanawaita walinzi hawa. Mimi sikuingia katika klasi, nilienda shule darasa la tatu. Hapa utapata wale wamepewa bunduki, wamemiliki bunduki kikabila. Kabila zingine zinatembea na fimbo tu, hapa sasa bila mshahara mtu ataweza kufanya kazi usiku nafikiri hawalipwi. Sasa pale ni kushindwa kwa Serikali, kumiliki bunduki, silaha ambayo ningependa mbele ya Tume iangaliwe sana. La sivyo watu wote wapewe bunduki ili wakati jambazi anakuja anajua yule mtu nikienda nitaanguka hivi.

Basi, upande wa umasikini, nashindwa ni nini inaendelea kwa sababu makampuni, utapata wale ma-M.D's katika ile kuhongwa wanawaajiri watu wao. Wamesahau mtoto wa masikini yule, hata hapandishwi cheo wengine wana retrenchment hata bila malipo, wanakwenda bure mikono mitupu. Wakafanya kazi wakachoka miaka sabini hawajachangia kitu N.S.S.F huko, watakula nini? Mzee akazeeka, tumbaku atatumia na nini kama hajawekewa pesa? Jambo hilo nafikiri liangaliwe kwa makini. Asanteni sana.

**Com. Maranga:** Asante kwa maoni yako na tutayatilia maanani kabisa, weka sahihi kitabu chetu rasmi. Andrew.

Atakayefuata Andrew ni Joseph Khoya, Joseph ako? Just a minute, Joseph ako? Okay, you will be next. Aah, thank you.

**Andrew Omuse:** Yes, kwa majina ni Andrew Omuse, Majune Catechist, Saboti Parish. Kwanza maoni yangu kwa Tume hii ni kwamba mambo ya kudharau imani ya makabila mengine katika Kenya tafadhali tunaomba ya kwamba isifuatiliwe sana. Mimi nasema kama Mteso kwa sababu Wateso wana mila zao na wakati inapofika wakati wa tohara, Wateso wanahangaishwa sana.

Jambo lingine ni kwa upande wa bursaries kwa ajili ya watoto masikini katika eneo letu. Twaona ya kwamba mtoto wa masikini ambaye anayesoma vizuri kwa sababu wazazi wake hawajiwezi twaona ya kwamba wanabaki nyumbani bila msaada wowote wa Serikali. Napenda Serikali ijayo kuona kwamba mtoto wa masikini mahali popote alipo, tafadhali asaidiwe na msaada wa elimu.

Pia, kwa upande ya makao tunaona kwamba kuna matajiri wengi sana katika nchi yetu ya Kenya….wana ekari tano kuonyesha ya kwamba umasikini umepata kutoka kabisa.

Na pia upande wa mambo ya kazi naona kwanza pia kuna watu wengi wamesoma na kwa sababu ya ukabila ambao tunao sisi twaona kwamba tukipata mtoto amesoma vizuri sana kwa sababu hana kabila lake katika ofisi ananyanyaswa na anabaki nyumbani bila kuchukuliwa katika idara yoyote. Basi, yangu namaliza kusema ya kwamba Mungu aweze kubariki Tume hii ya Katiba, asanteni.

**Com. Maranga:** Aah, asante sana Joseph kwa maoni yako…

**Andrew:** Thank you, ni Andrew.

**Com. Maranga:** Ningekuomba tu uweke sahihi kitabu chetu rasmi, thank you very much. Anayefuata ni Coleta Cheruandui, Coleta Cheruandui next. Halafu atafuatwa na Jacqueline Naibei, Jacqueline ako?

**Coleta Cheroandoi:** Kwa majina ni Coleta Cheroandoi. Natoka Tavoti Division katika Location ya Kinyoro. Maoni yangu ni kuhusu tu laini za akina mama haswa tumenyanyaswa. Kina mama tunapoenda kama mfano wakati wa masiasa tunapuuzwa na wanaume, tunatukanwa, tungelipenda nyinyi watu wa sheria mtupatie sheria yenye wanaume hawawezi kutupuuza mbele ya watu ili itulinde tuwe pia na uhuru. Kwa ajili hiyo kitu inawawezesha akina mama hawako free kufanya kazi vile wangelipenda.

Lingine ni wazo hili, hii maneno ya culture na tohara tungelipenda haswa Sabaoti culture tungelipenda hiyo tohara tuache na hebu mtuachie kwa ajili sisi wenyewe tutamaliza vile tulianza sisi wenyewe bila ya watu wengine kuingilia wenye hawajui maneno ya hiyo kimila. Hebu watuachie halafu sisi wenyewe tumalize.

Tume ya Kurekebisha Katiba sina mengi lakini ningelipenda sheria ya kutunza akina mama nchini Kenya mtusahau wakati ile zingine haswa wakati mwingine tena kabla sijamaliza nilikuwa karibu kusahau. Kabla ya uhuru Kenya, akina mama tulikuwa na watoto na watoto wanaume wenye tulizaa na hao walitusaidia. Na wakati huu wazee tunazaa nao watoto wanatupuuza, watoto wanajaa kwa streets wakisema ni wa wanawake na iko wale wanaume tulizaa na hawa. Tunataka sheria ya kushikia sisi hawa wanaume tulelee hawa watoto pamoja. Kwa hivyo sina mengi, nimeshukuru kwa hayo.

**Com. Maranga:** Nina swali moja. Kwa hivyo unataka tohara ya wasichana iendelee?

**Coleta:** Isiendelee lakini watuachie vile tulianzisha sisi wenyewe tukatishe pole pole.
**Com. Maranga:** Kwa hivyo unasema iendelee nyinyi ndio mtaamua vile itaisha?

**Coleta:** Hapana, tunataka iishe lakini sisi tuendelee kwa ajili iko akina mama wengine wasi…

**Com. Maranga:** Aa aah, wacha nikuambie, wewe unasema msituingilie kwa hiyo tohara, tunataka iishe pole po..

**Coleta:** Pole pole.

**Com. Maranga:** Na tena unasema hutaki iendelee. Kwa hivyo mimi nataka utupe ukamilifu kabisa, uambie Tume unatakaje iendelee ama isiendelee?

**Coleta:** Isiendelee lakini mwenye hajapashwa tohara asiambie mwenye alitoshwa tohara kwa ajili haelewi.

**Com. Maranga:** Okay, asante. Thank you very much.

**Coleta:** Asanteni nanyi.

**Com. Maranga:** Okay, weka sahihi hapo. Eeh, hii ndio tunasema mjadala wa katiba ama namna gani?

**Wote:** Ndio.

**Com. Maranga:** Hiyo unapeana kwa ule ama hii ni copies? Ni copies, okay thank you very much, umepeana kwa…kwa Mohammed?

**Speaker:** Nitapeana.

**Com. Maranga:** Mpa yeye, huyo ndio mtu wa muhimu anatuwekea hapo kabisa, Jacqueline Naibei.

**Jacqueline Naibei:** Wacha niongee halafu ataa… Naitwa Jacqueline Naibei kutoka Kisawahi na nafikiri yale ambayo wenzangu wameongea haswa mama Coleta tumekuwa tumekaa na yeye karibu na yameongewa yale labda ningeongea ingawa ninaweza kufafanua kidogo juu ya vile amesema juu ya tohara.

Nataka kusema hivi, kwa wale communities ambao labda hawa-practise hayo mambo ya tohara kwa wasichana, tohara kwa wasichana sisi Wasabaot tumeona sio nzuri ijapokuwa isiwe ni kitu ambacho imesemwa tu ovyo ovyo mpaka kabila zingine wanaona kwamba haikuwa na umuhimu wake. Nataka niwaambie hivi na labda wanaume wa Sabaot wakiwa hapa na wamama wanaweza kunikubalia ya kwamba tohara kwa wasichana Wasabaot mbeleni ilisaidia sana wasichana wa Sabaot. Wangeweza kuolewa wakiwa mabikira kwa sababu kuna vitu vyao ambao walikuwa wakiambiwa ya kinyumbani yenye walikuwa wakifuatia na wanaitilia mkazo, wanaitilia maanani mpaka siku ile msichana ataolewa bila kuonana na mwanamme na hiyo ingesaidia sana. Tungepata wasichana Wasabaot wengi hawakuwa wamezaa nyumbani ovyo ovyo. Kwa hivyo nataka kusema hivi, sipingi kwamba hiyo kitu iendelee lakini sisemi ya kwamba iendelee lakini isiwe ni kitu ambaye inaongelewa tu na kila mtu ovyo ovyo kutangazwa ovyo wachia sisi wenyewe tuseme mambo yetu nyumbani.

Ingine, nasema ukweli kwa sababu hiyo kitu ikiwa ni kitu isiwe ni kitu inafinywa halafu…

**Com. Maranga:** Patia yeye nafasi, patia yeye nafasi, wacha atoe maoni yake nyinyi mtatoa yenu.

**Jacqueline:** Si vizuri sana uongelee ile kitu huelewi ama hujui. Sisi wenyewe tunaweza kusema nyumbani hapa ni mbaya hapa ni nzuri kwa ajili ya hii na hii na hii. Tunaenda kanisa, tunaenda shule, tunajua umuhimu yake ama ubaya wake. Kwa hivyo wachia sisi sio mtutangaze ovyo ovyo maana itafikia mahali hata wasichana wengine wa kabila zingine watatudharau waone sasa tulikuwa tunafanya vitu ile useless na sisi wenyewe tulijua umuhimu wake.

Nataka kusema tena hivi, kuna mama alisema saa zile juu ya urithi. Kweli, sisi mimi nataka kusema kama mama ya kwamba akina mama tumeumia kwa upande ya urithi. Mwanamme akifa mama anang'ang'aniwa na wanaume wa boma hiyo kwamba anataka kurithi maana mali yao ilifanya nini, ilipeanwa. Na unaona inaumiza wamama wengi wamepoteza vitu vingine hata watoto wengine hawasomi kwa ajili ya kulazimishiwa. Kama kitu au…kama labda urithi itaendelea kwa watu wengine na kama labda mtu amependana na shemeji yake kimapenzi vile labda alipendana na mume wake, isiwe kitu ya kulazimishiwa. Mama mwenyewe aamue kwa upande wake.

Na kuna ingine tena nilitaka kusisitiza. Ingawa hii ilikuwa ni kitu imesemwa ni kwa ajili ya hawa watoto ambao wamezaliwa nyumbani na wasichana wetu ama na wamama wenye hawajaolewa. Nataka kusema hivi, wamama wengi wameumizwa na

wanaume kwa njia hiyo. Watoto wengi wamezaliwa mtu anazalia mama watoto karibu tano hana makao, ana-rent nyumba labda ya shillingi mia mbili anaenda kibarua, na huyo mtu hajali na anaita ni watoto wake kimadharau tu, hata hawezi kujali aseme wacha nipeleke hawa watoto shule ama hata wacha ninunue nguo. Kama sheria ingewekwa ya kuchukulia hawa wanaume hatua kali nafikiri hata mambo ya usherati ingekuwa imepungua hata Ukimwi haingekua inaendelea. Kwa hayo machache nasema ni asante.

**Com. Maranga:** Basi hayo ni maoni ya mama Naibei, asante. Kwenda uweke sahihi, kwenda weka sahihi kitabu chetu rasmi. Kuna Joseph, nani yule alitoa maoni? Kuna hitilafu ya jina hapo, ni nani yule ali-appear?

**Wote:** Andrew.

**Com. Maranga:** That was Andrew, so Joseph hajatoa? Haya, sasa wakati ni wako, dakika tatu mzee wangu. Toa maoni ya muhimu naona umetupatia memorandum kubwa kabisa. Toa ile maneno ya muhimu, asante.

**Joseph:** Nashukuru kupewa nafasi, ingawa haitoshi. Kwanza Constitution hii ni ya muhimu kuliko zote ambazo zimewahi kufanyika hapa Kenya. Unaelewa 1963…

**Com. Maranga:** Ungeanza na majina yako kamili.

**Joseph Khaoya:** Majina yangu ni Joseph Khaoya, Joseph Khaoya, E.B.S. Hii ndiyo ya muhimu kuliko zote ambazo zimefanyika. 1963 tulikuwa na majadiliano Lancaster lakini hiyo walikuwa wanabishana tu kuona wazungu wanatetea mali yao namna gani na sisi Waafrika siku hizo tulikuwa saa yote tunapiga simu Lancaster letea sisi uhuru wa aina yoyote. So, nobody ever took into consideration the common man’s affairs.

Ile ya 1966 ambayo nilikuwa huko kwa Bunge ya kwanza, it was to revise na kuvunjilia mbali maneno ya Majimbo na hakika Wakenya hawakuuliza maneno ingine kuweka kwa Constitution. Kwa hivyo, hii ndio mimi naonelea ni Constitution ambayo inaweza Wakenya tukaketi na tukatoa moja ambayo inaweza kulast 500 years from now. Na ndipo nasema lazima mwende pole pole mpewe nafasi ya kutosha, kama hamwezi kumaliza this year, mpewe nafasi next year na kama kuna shida hata Bunge iongezwe maana nina mfano in 1966, wakati tulikuwa tunajadiliana hii mambo ya majimbo na kuondoa majimbo, Bunge tuliamua tukaongeza miaka mbili zaidi kutoka 1967 kura ikapigwa 1969. Kwa hivyo isiwe iko kelele kabisa nyingi katika nchi pengine kufikiria Bunge kuongeza muda yao na ya Commission kuna makosa. Hakuna makosa bali mimi vile naona hii Wabunge wangependa kujiongeza mishahara mara kwa mara ikiwa wataongeza Bunge na hatuwapi ruhusa kuongeza mishahara kwa hiyo period of extension.

Nazungumza juu ya future President – Tunaye President wetu mtukufu mpendwa amefanya kazi yake karibu sasa miaka ishiri na

nne. Na ingawa tunasema two terms of five years each making a total of ten years, this is somehow misleading wakati inaenda kuwa applicable kwa Presidents ambao watakuja siku zijazo. Kwa hivyo ningeonelea kwamba vile tumeona mungeweza tume tumeona hapa mkate vile anafinyana, miaka kumi imekwisha hata kuna mapambano huko, tungepeana term tatu kwa ma-President ambao watachaguliwa baada ya President wetu mtukufu Moi. Ni maneno mengi na kujaribu kusukuma kwa dakika tatu is almost impossible. Lakini mzee Moi, wakati wake ukija unakuja mwisho mimi kama mzee mkongwe naonelea lazima tupeane retirement package ambayo inaweza kufanya huyu Mzee akaenda akaketi vizuri. Moja ni kwamba akimaliza Bunge na kazi ya Urais kwa miaka tano ambayo inafuata, mtu yeyote asipeleke yeye kortini ya Kenya. Hii itampa peace of mind apumzike kama mzee. Apewe pia mshahara wa kutosha kujilinda kwa uzee wake na pia apewe security ile ambaye mwenyewe anachagua ili wasije wakaingiza masecurity ambayo watamaliza huyu Mzee wakati analala usiku. Tunataka tu wale security ambaye anapenda na baadaye nasi tuulize kwamba awachane na maneno yote asiwe running commentary kwa vile President ambaye tutakuwa tumechagua,eeh? Aketi na hata asijaribu kusaidisha sisi kupata next President, hapana, sisi tumpe heshima yake na aende aketi sisi wenyewe Wakenya tupambane kutafuta President mwingine.

Na jambo lingine ambalo nataka kusemea kwa ufupi ni kwamba appointment na dismissal ya Ministers and Assistant Ministers, appointment ni maneno ya furaha lakini tumeona mara nyingi Minister iko kwa Government function yeye ako kati kati anaendesha halafu sijui redio saa saba kawaida hii maneno ambaye inatokeanga saa saba ya mchana. Redio mtu ameketi kwa gari hapo na anatoka huko kwa gari anapeleka kabarua kidogo kwa huyu Minister ambaye iko kwa kazi, anaambiwa unasikia? Saa saba wametangaza wewe umefutwa, eeh? Wewe umefutwa na maneno inaanza mara moja. Wengi wame-collapse. I have been an Assistant Minister myself before and I know how painful it can be, it can be very painful. Wewe unaona mtu anaanguka tu, hujui anaanguka nini, opponents wake ndio wanapata nafasi ya kucheka na kusherekea, si tulisema, eeh? Vitu kama hivi, we have to be civilized about dismissing our Ministers in future. That kabla matangazo yoyote kwa redio, huyu apeanwe awe served na ile karatasi ya dismissal ndio baadaye hata wakitangaza kwa redio, pia yeye yuko tayari. Otherwise, it is a very uncouth way of dismissing our leaders.

**Com. Maranga:** Last point, Sir.

**Khaoya:** Sorry, I have two points. One is food security and the other one is squatter problem. Now, very briefly food security inataka kwamba future Government wasipewe wasipewe nafasi ya kuchezacheza na staple food yetu ikiwa ni mahindi, ikiwa ni maharagwe…

**Com. Maranga:** Aah, tafadhalini muende pole pole unajua tunafanya recording na hiyo sauti itakuwa recorded na hamtaki maneno ya Sabaoti tuseme ilikuwa sauti tu na hiyo ni viti mnavuta. Chukueni pole pole ndio msongee, sawa sawa. Asante kwa kuheshimu hiyo. Endelea.

**Khaoya:** Future Government wasipewe ruhusa ya kuchezacheza na mimea yetu ikiwa wanafanya urafiki na COMESA ama na

wengine mpaka ikasababisha hali ambapo tuko watu wa Trans Nzoia saa hii bei ya mahindi imeenda chini maana Serikali yetu imefanya urafiki na mahindi bei rahisi ya shilingi mia mbili inatokea Uganda, eeh? Kwa hivyo in future no Government shall be permitted kufanya urafiki na nchi zingine wakifanyia urafiki mmea wetu ambao ni staple food na staple food inatambulika kama mahindi siku hizi, maharagwe na hivi viazi vya kizungu. Pengine tunaacha ingine.

Kwa hivyo la mwisho ambalo nataka kusemelea, Wazee mnisamehe, ni hii squatter problem which is as old as the history of Kenya maana squatter ilikuwa wakati wazungu walikamata White Highlands, walitaka watu wawasaidie kazi na hapo ndio squatter ikatokea. 1931 Carter Commission iliingilia jambo hili hata wakazungumza juu ya wanaosha wafanyi kazi, mzungu akapewa ng'ombe mbili ya maziwa ama nini? Wakafikia maneno kama hiyo, wapewe 1/6th of an acre, eeh, na ng'ombe mbili ndio ulikuwa unasikia zamani kwamba nimekata blue. It was because certificate hiyo ilikuwa rangi ya blue na ile mechanization imeingia kwa wingi, matractor sasa watu hawatakiwi wengi na vile ng'ombe za kizungu zinaingia exotic breeds, hivi vitu vikawa vinafifia. Ikawa sasa ni Mwafrika ndio ananunua shamba la mzungu na katika maandishi, free of encumberances na nyinyi kama mawakili mnajua huwa sasa mtu amenunua shamba lakini hanunui ma-squatter. That is the problem mnayo na ikiwa tuna haja ya kumaliza hii, tunaimaliza. Ikiwa tunaamua leo na Commission kwamba wale watu ambao walikuwa Saboti Constituency ama Trans Nzoia, watu ambao walikuwako watu wazima, 18 years and above the year of our Lord 1963 ndio wakati tulikuwa tunapata independence. Ikiwa watu wale tunaingia na kutambua na mimi nitakuwa mmoja wa kusaidia kutambua hawa, ikiwa wanatambulika it is possible kuwapa mashamba acre moja moja, not acre, hectare that is 21/2 acres. Kila mmoja apewe hiyo, yeyote alikuwa Trans Nzoia wakati tulikuwa tunapata uhuru kila mmoja apate hiyo, it can be done. Lakini kosa ni kwamba wale ambao wanaulizwa sasa kwenda kupeana kama D.C, D.C anajifanya yeye ni squatter anakamata acre mzima, eeh? Kama Minister, unaona Minister hapo hata Attorney General hata nani. Hawa ni ma-squatter ya Trans Nzoia wanakamata acre hamsini, acre mia moja, this way we can never do it. Nafikiri lazima tupeane nafasi hata ikiwa ni muda mfupi, Commissioner of Squatters hata mimi nipewe hiyo pesa. Six months tutakuwa tumemaliza hiyo shida ya squatters halafu tuwe na kazi ya wengine ambao watakosa mashamba kutokea hapo, maana tunachanganya wale ambao walikuwako na wale wengine ambao wameuza mashamba yao tena wanaenda sokoni. Na ukiuza sasa shamba ukaenda sokoni ati uitwe squatter mpya, hii si kweli, tunataka wale wote ambao walikuwa. It is really not fair, tumepata independence na watu ambao pia walikuwako wanapata independence aendelee kuwa squattor kwa Khaoya kwa miaka thelathini ingine, I feel very painful, very painful indeed.

**Com. Maranga:** Asante Mheshimiwa.

**Khaoya:** Asante

**Com. Maranga:** Unajua umeenda juu sana na nimekuheshimu kwa sababu ulikuwa Mheshimiwa na nikuheshimu sana,

**Khaoya:** Tena ni Mzee ya zamani

**Com. Maranga:** Na tena ni mzee ya zamani. Haya, sema la mwisho.

**Khaoya:** La mwisho ni poverty eradication. Hii bila access kwa kaloan kidogo kwa wakulima hawa wataendelea kuwa masikini year after the other. Maana unaona sasa ukipita hapa kwa njia Bwana Commissioner utapata asubuhi wakina mama na watoto wote wanabeba majembe wanatembea kwa barabara wanatafuta kazi. It is very painful. If these people could be given small loan ya kulima acre tano na ajilipe mshahara mwenyewe kutoka kwa ile kaloan yeye aweke mbolea ya kutosha, eeh, apalilie mahindi yake sawa sawa acre mbili acre tano apate kama magunia mia mbili hivi, that would be about 200,000 shillings tutakuwa tumemaliza hii na bila A.F.C kurudi in place, we are in trouble. Tafadhali na-recommend A.F.C or any other organization like it ipewe nafasi na wakulima waendelee kupata pesa kidogo dogo, mbolea, seed kupalilia hata kupata kanyama kidogo unaandika ndani ni kupalilia lakini si wewe ndio unaenda kupalilia, kanyama kidogo….

**Com. Maranga:** Asante Mzee wangu, asante…

**Khaoya:** Asante sana, thank you very much.

**Com. Maranga:** Asante na tumeshukuru kwa maoni yako. Eeh, wananchi nimempa dakika chache tu juu kwa sababu yeye ni mzee na alikuwa kiongozi kwa hivyo msione ubaya sana, asanteni. Basi Mzee tupe hiyo memorandum na ujiandikishe. Abraham Chebet is the next. Atafuatwa na Pastor Peter Kimaswet, ako? Pastor ako? Basi uwe tayari sana, huyu akitoka uwe karibu. Watu ni wengi na hatutaki mtu akose nafasi ya kuongea mbele ya Tume.

**Abraham Chebet:** Yes, kwa majina naitwa Abraham Chebet na langu Bwana Commissioner Sir ni jambo ambalo limenitatiza kwa makaazi yangu ya kwamba ningependa through you Bwana Commissioner nikwambie jambo ambalo linatutatiza.

Jambo hili lenyewe ni hotuba ambayo ilitolewa mradi tu Waziri Mkuu wa kwanza katika nchi hii alipohutubia watu wananchi juu ya ardhi. Yeye ilikuwa alitoa hiyo hotuba tarehe 5 Februari katika uwanja wa Kamukunji Stadium, tarehe 5 Februari 1962. Jambo hilo ndilo jambo ambalo linatatiza sana kuhusu mambo ya ardhi. Yeye alisema hivi, ningependa nisome hiyo kama in quotation Bwana Commissioner Sir. Alisema ya kwamba, "Mimi ninawaambieni mjihadhari kwa sababu watu wengine watakuja kuwadanganya. Ooh nchi yako itachukuliwa na Wakikuyu, nchi yako itachukuliwa na Wajaluo, nchi yako itachukuliwa na Wakamba, mitasadiki mambo hayo? Na jawabu ilikuwa ni kwamba hapana. Katika Constitution, katika katiba mpya Serikali yenu imeahidi kwamba kila sehemu ya nchi kama ni ya Maasai itakaa kama hivyo. Itatawaliwa na Wamaasai wenyewe, kama ni nchi ya Wakipsigis itakaa ikitawaliwa na Wakipsigis wenyewe. Kama Wanandi, Wanandi ndio watakao watatawala nchi yao, hiyo ni kusema ardhi yao. Hakuna mtu kutoka nje kwenda kunyang'anya mali yao, mashamba yao ni shauri yao kujua watafanya nini".

Kwa hivyo, Bwana Commissioner Sir, pendekezo langu ambalo ningependa nitoe pendekezo kufuatana na hii vile ninasema

mimi ni mmoja wa wale, mtoto yule alifanywa kuwa squatter katika ardhi ambayo ilikuwa ni yake na nimekuwa kama mtoto squatter. Na kufuatana na hiyo hakikisho ya makabila kwa ardhi yao, ningependa nipendekeze hivi Bwana Commissioner ya kwamba the Pre-independent land treaties or forceful acquisition of ancestoral or traditional land must be removed and the land in question returned to the Pre-independence owners. This was accepted wakati walipokwenda katika Lancaster hata wakati wa hao majimbo ilikubalianwa kwamba wao wenyewe na hiyo ndiyo ilikuwa jambo ambalo watu walikuwa wakipigania.

Kwa hivyo hata yule Waziri Mkuu alisema hivi, “Our greatest asset in Kenya is land. This is the heritage we received from our forefathers. In land lies our salvation and survival. It was in this knowledge that we fought for the freedom of our country”. Kwa hivyo mimi napendekeza the indigenuous mimi kutoka jamii ya Wasabot ni mmoja wa wale ambao tulikuwa tunaishi hapa katika Trans Nzoia ambapo shamba au mashamba ilinyang’anywa na wazungu wakafanya sisi kuwa landless up to death. Sabaot community have not been given the schemes wakati tulipopewa uhuru, watu wale ambao walikuwa squattors walipewa settlement schemes katika jamii hii hatukupewa. Kwa hivyo hilo ndilo jambo ambalo naona ni kwamba ni chungu sana ikiwa Serikali imekubali nyinyi kuja hapa naomba kwamba tuwe na katiba ambayo itafikiria na kurudishia indigenuous land yao. Hiyo ndiyo mimi naomba.

**Com. Maranga:** Asante Mzee Chebet. Ile tu swala ningekuuliza kabisa pengine ungechukua muda mfupi kabla hatujamaliza kuchukua maoni ya Tume uandike historia fupi kuhusu hii shamba kwa sababu hatuwezi tukajua kila makabila kwa mfano, Nairobi inasemekana ilikuwa ya Wamaasai. Sasa Nairobi inakaliwa na kila kabila ya Kenya na Wahindi na kila mtu, tunaelewana?

**Chebet:** Yes.

**Com. Maranga:** Sasa pengine ungetuambia hii historia unataka hii indigenuous land iende urefu nyuma mpaka hadi lini, tunaelewana? Ni miaka gani unataka uweke kama mark kwa sababu kila watu wanasema tulikuwa tunakaa hapa miaka fulani, wengine miaka fulani, tunaelewana?

**Chebet:** Nimekuelewa.

**Com. Maranga:** Sabaot wakati wazungu walikuja maybe ndio walikuwa wanakaa
hapa,

**Chebet:** Nimekuelewa.

**Com. Maranga:** Tunaelewana?

**Chebet:** Tunaelewana.

**Com. Maranga:** Kwa hivyo tupate historia…

**Chebet:** Kwa hivyo…

**Com. Maranga:** … ndio wakati tunajaribu kurekebisha tuone tunafanya nini.

**Chebet:** Asante sana Bwana Commissioner.

**Com. Maranga:** Okay.

**Chebet:** Jambo ambalo ninge nitakujibu ni kwamba hiyo historia tunaweza kupa hata leo.

**Com. Maranga:** Very good.

**Chebet:** Asante sana.

**Com. Maranga:** Basi utupatie.

**Chebet:** Thank you.

**Com. Maranga:** Thank you very much, andikisha na utupatie memorandum. Aah, Pastor ako wapi, Pastor? Tafadhalini muwe kwa haraka kwa sababu watu ni wengi hatutaki kupoteza muda, Pastor Peter Chemaswet, ndio sababu naita watu mapema. Eeh, anayefuata ni Hon. W.A. Kisiero, Mheshimiwa ako, Mheshimiwa? Basi uwe karibu hapa Mheshimiwa wakati huyu anamaliza uingie show, thank you. Aanza kwa majina Pastor, karibu.

**Pastor Peter Chemaswet:** Mimi naitwa Pastor Peter Chemaswet wa Kanisa la Baptist.

**Com. Maranga:** Endelea.

**Pastor Peter:** Langu leo hii nashukuru ya kwamba Tume hii imefika mahali hapa kwa ajili ya kuchunguza mambo ya kutengeneza Katiba mpya katika nchi yetu. Ni jambo lililo nzuri ni kitu ambacho tumepewa nafasi safi ili ya kwamba tukapate kusema mambo yetu kulingana na vile tunavyohitaji. Langu ni kusema ya kwamba katika Katiba hii tunahitaji Katiba ambayo itatambua haki ya watu wote kuishi bila ya masumbuko. Na Katiba hii itambue swala la ardhi haswa jambo ambalo limeletwa

na mzungu na shida yote ikaingia mpaka wakati huu na ndio maana tumekuja kujaribu kurekebisha. Yale ambayo tunajaribu kurekebisha ni matatizo ambayo yaliletwa na mkoloni kwa sababu mkoloni alipofika mahali hapa alikuta ya kwamba watu walikuwa wanakaa bila shida ijapokuwa walikuwa na shida tofauti tofauti lakini matatizo ambaye alileta baadaye ndiyo maana tumekuja kuyarekebisha.

Kwa hiyo, ningependekeza kwamba Katiba ambayo itakayoundwa itatambua haki ya wale watu ambao wanaitwa minorities, walio wachache katika maeneo ambayo wamo ndani. Hasa tunapoangalia katika eneo hili la Trans Nzoia tunaweza kuona ya kwamba watu kama Wasabaot ni watu ambao mzungu alimwondoa mahali hapa na aka-create yale ambayo yanaitwa Whiteland Slums na kwa hiyo ingefaa ya kwamba haki ya hawa watu ambao waliotawanywa ikapate kutambuliwa na wapate kupewa sheria itakayolinda kuishi kwao mahali hapa na hii ni kusema kwamba Katiba hii ambayo tunahitaji iwe ni Katiba ambayo itatambua na kurekebisha ile Katiba iliyokuweko 1962 ambayo ilikuwa inazungumzia mambo ya Majimbo.

Na ninaposema ya kwamba mambo ya Majimbo, simaanishi ya kwamba watu wakapate kuhamishwahamishwa na ili ya kwamba original people wapate ardhi yao, sio hivyo. Namaanisha kwamba watu hawa wapate kuishi pamoja kwa amani na haki ya yule aliyekuwepo sheria ikapate kumtambua na wapate kuweka special priorities ili ya kwamba wakapate kukuwa na representatives katika Parliament na hiyo namaanisha kwamba wawe na nomination wapewe kwa sababu wakienda kwa mambo ya kura hawataweza kwa sababu wao ni wachache. Kwa hiyo hii Katiba ikatambue hawa watu, wapewe special eeh, vile ilivyokuwa katika wa 1960's kulikuwa na huyu Bwana ambaye aliyekuwa anaitwa Chepchikit, kuna kitu kama ile ilikuwa imewekwa mahali hapa Trans Nzoia. Kwa hiyo ndio naomba ya kwamba wapate ku-create jambo kama hilo ili hawa watu pia wawe na representatives katika Bunge yetu kwa new katiba mpya.

Jambo la pili ambalo ningezungumzia ni ya kwamba Katiba hii ikapate kutilia maanani na kuweka sheria iliyo kali juu ya jambo ile ambaye inaitwa corruption kwa sababu corruption imeleta shida. Watu wakipewa ardhi utagundua ya kwamba wale wanaohusika kutambua na kuweka watu wapate kupata ardhi wanaingia katika mambo ya rushwa, wananunuliwa ovyo ovyo hata wengine openly wakionekana wakipewa hela. Na kwa hiyo ina na wale wanaotakikana kuingia katika ardhi ile hawaingii, wale wakubwa wakubwa wanaingia. Kwa hiyo naomba ya kwamba Katiba hii mpya ikapate kutilia maanani jambo hili ili ya kwamba atakayehusika na kuvunja sheria kwa kuchukua hongo wakapate kuwekwa katika eeh kuchunguzwa vizuri.

**Com. Maranga:** Ya mwisho Pastor,

**Pastor Peter:** Naam.

**Com. Maranga:** your last point. Hata umepita dakika tatu.

**Pastor Peter:** So, asante.

**Com. Maranga:** Lakini maliza ya mwisho, ya mwisho.

**Pastor Peter:** Ya mwisho, ningeomba ya kwamba kwa sababu iko Katiba inakuja, naomba ya kwamba katiba hii ikapate kuruhusu watu kama Mt.Elgon District ikahamishwe ije sehemu za Rift Valley Province kwa sababu mzungu aliwagawa hawa watu na wakagawanyika. Kwa hiyo naomba ya kwamba ikapate kuletwa huku kwa maana watu wanapoimba na kuzungumza huwa wanazungumzia mambo ya ardhi yao na inatakikana iwe hivyo. Ya kwamba wakapate kuhamishwa waje katika eneo hili la Rift Valley Province.

**Com. Maranga:** Asante, aah hata ingawa sikusikia wewe vizuri sana Pastor, wewe ni mchungaji wa watu wengi, unapendekeza nini kuhusu shamba?

**Pastor Peter:** Juu…

**Com. Maranga:** Tunataka very specific recommendation in one sentence.

**Pastor Peter:** My recommendation about land is this, ya kuwa ardhi ambayo imebaki ipeanwe wakapate kurudisha nyuma kidogo mpaka 1900. Wale ambao wazungu waliwahamisha kutoka mahali hapa mahali popote walipo before the year 1900, nani alikuwa mahali pale? Na iwapo hao watu wapo kwa wingi na hawana mashamba, wapewe kipao mbele moja. They should be reconsidered first.
Ya pili ni ya kwamba iwapo kunao wengine pia ambao walikuja probably baada ya independence na wako squatters, wapate kuangaliwa pia kwa njia ya proportion.

**Com. Maranga:** Asante, asante sana nakuomba sasa uweke sahihi kitabu chetu rasmi.

**Pastor Peter:** Thank you.

**Com. Maranga:** Thank you kwa maoni yako. Mheshimiwa Kisiero, I know you have a good memorandum and you are an honoura…a former Honourable Member of Parliament. Please, I am going to request you to summarize your main points in three minutes.

**Hon. Kisiero:** Thank you very much

**Com. Maranga:** Thank you, Sir. Yeah.

**Hon. Kisiero:** Thank you Mr. Chairman, Sir. Eeh, la kwanza,

**Com. Maranga:** Start with your names.

**Hon. Kisiero:** Ooh, Jina langu ni Wilberforce arap Kisiero ambaye alikuwa mjumbe hapo awali na pia Assistant Minister. Jambo la kwanza Bwana Chairman ni kwamba shida ambayo iko Kenya wakati huu ambayo imetufanya kuwa na kamati hii yenu ni kwamba President, presidency is the breeding ground of the problems and this is where the problems are. The Constitution has given the President too much powers including giving out posts and all, appointments of Ministers and what have you and therefore everybody else is fighting to get that position for his tribe because Kenya basically is still ethnically composed. Bado tunafikiria mambo ya ukabila sana.

**Com. Maranga:** What do you recommend, Mheshimiwa?

**Hon. Kisiero:** Na-recommend ya kwamba nguvu za President zigawanywe, tuwe na Prime Minister na pia kuwe na President lakini nguvu hizo zigawanywe ili mmoja wao asiwe na nyingi sana. Na hiyo itapunguza wengine ambao wanataka kuja ambao wanataka kung'ang'ania kwenda ku-protect interests za makabila zao.

La pili ni kwamba ukoloni ulileta uchafu maana walipokuja wakaingia wakanyang'anya wale waliokuta, walipoona mchanga mzuri kila kitu nzuri wanafagia kama vile walifagia Wasabaot kutoka Trans Nzoia, na walipoondoka hawakukumbuka kumrudisha yule waliyemfagia. Kwa hivyo hiyo imefanya watu wengine kujifikiria hawatakiwi, ukoloni iliwafagia na pia Serikali pia haikuwasaidia. Tunataka Serikali iangalie indigenuous tribes in various parts of Kenya, waangaliwe haki zao.

Lingine Bwana Chairman ni kwamba tungetaka kuwe na some kind of devolution of powers sio ya Prime Minister peke yake na kugawanya na President. Tungetaka County Councils, Local Authorities wapewe nguvu zaidi ili waweze kutekeleza kazi vizuri bila kuingiliwa.

Lingine Bwana Chairman ni kwamba tungetaka pia Constitution jinsi imeandikwa iko taabu kwa maana wamesema wamempa mtu rights zake, walisema wamepeana basic rights ya kwamba unaweza kwa mfano nitasema moja tu Chapter 5 of Section 78 of the Constitution juu ya kuabudu. Wanasema una haki kuabudu uwezavyo na Constitution ndio supreme lakini unakuta kila wakati watu ambao wanaitwa Seventh Day Adventists wakikataa kufanya kazi siku hiyo ama watoto wakikataa kusoma siku hiyo wanafukuzwa. Juzi watoto walifukuzwa Kapsabet, wasichana wengi ambao ni S.D.A na D.O mmoja kwa maana Madaraka iliingia siku ya Jumamosi akakataa kwenda akafukuzwa na hali Constitution inasema we have protected you. So, look at the limitations provided in the Constitution in various parts of the Constitution maana wanampa wewe Constitution halafu wananyang'anya tena huko nyuma. Surely, school rules are not better than the Constitution. Na huyu mtu ambaye anasema conscience yake inasema nataka kuabudu aheshimiwe kama vile Constitution inavyotaka.

Bwana Chairman Sir, nilivyosema juu ya reversion eeh sijataja Reversion Rights. Katika Lancaster House, katika Lancaster House walipofanya mkutano kabla ya mkutano kulikuwa na Secretary of the Colonies. Alikuja Kenya na tarehe 29 November alisema ya kwamba the great danger…

**Com. Maranga:** In which year?

**Hon. Kisiero:** Ooh sorry, 1961, Mr. Chairman. Alisema alipokuwa akirudi Uingereza na akatangaza ya kwamba Conference ya Lancaster ingefanywa tarehe 14 mwezi wa pili, mwaka wa sitini na mbili. Alisema, "The great danger I see is fear, fear of discrimination, fear of intimidation, fear of exploitation I have seen enough to be convinced that there is truth underlying these fears".

Tungetaka Constitution ambayo mtajaribu kuandika iondoe hofu, hofu bado iko. Kama nilivyotaja makabila kubwa kupigania viti vikubwa iko kabila hizi ndogo ndogo ambayo wanakanyagwa vile kama ndume wanapokanyaga tu grass. Hawa makabila muangalie kwamba wapewe nafasi katika system ya election ili waweze kutengewa viti ambavyo wataweza kuzipata kwa urahisi. Some kind of proportional representation but within the usual the usual plurality system ya election. Those areas where those minorities are kama Sabaot waweze kutengewa special seats not only in Parliament, also in Local Authorities and other elective positions so that fear is also removed. Fear of domination, they are small they are unable to compete but once you do that you give them also hope. They are part of Kenya.

Ulikuwa umemuuliza mwenzangu mmoja aliyezungumza ya kwamba ungetaka kujua historia fupi ya mambo ya Wasabaot. Sijui kama utaniongeza muda nikueleze lakini nimeweka summary tumeweka summary kidogo katika hii memorandum ya community,

**Com. Maranga:** Okay.

**Hon. Kisiero:** Tumeweka kidogo lakini kwa ufupi ni kwamba…

**Com. Maranga:** Historia ya Wasabaot in relation to the land in Trans Nzoia.

**Hon. Kisiero:** To the land in Trans Nzoia and how they have been removed and how they are suffering in small…

**Com. Maranga:** I give…

**Hon. Kisiero:** But we are going to give you more information if you need but something is mentioned here.

**Com. Maranga:** But give me a mentioning in a minute.

**Hon. Kisiero:** Yes Mr. Chairman, Sir. Sabaot walikuwa ndio indigenuous wenye kukaa Trans Nzoia. Wazungu walipokuja walirecord ya kwamba Sabaot ndio wenyeji, iko katika records na Commission ya kata ya 1932, ni Sabaot pekee yao ndio wali-appear katika Commission wakiulizwa watakuwaje kwa maana wazungu walitaka kuwaondoa. Wakaja 1932 wakapeana maoni yao, wakalia, wakasema jameni mmetunyang'anya lakini wakaambiwa hapana ninyi enda Uganda maana ninyi mnasema Kisebei na iko maandishi iko, records zote ziko available everywhere. Wakahamishwa wengine wakaambiwa ninyi mnafanana na Wamasai kwenda na Wamasai, wakahamishwa na Wamasai, wako Kilgoris wamekuwa nusu Masai nusi Sabaot. Wamasai waliokuwa unfortunate wakashikwa wakapelekwa Mt.Elgon na Bungoma.

Walipokwenda huko wamekuwa Waluhya na wamekuwa Wasabaot, wamepotea. Kwa hivyo kwa vile jameni mgeni anakuja anakutoa anakutimua lakini alipoondoka, si angesema eeh mzee, rudi mimi nakwenda. Hakufanya hivyo jamaa akasahau akafunga mizigo akatoroka bila kutualika. Kwa hivyo imewafanya Sabaot wanaishi kama mbwa, they are all over the place, they are just destitutes. Hatutaki, hatusemi mtu afukuzwe, tunataka Constitution irecognise the rights of the indigenuous the way other Constitutions have accepted in the world. The Canadians have done it, the Americans have done it, the Phillipines have done it and there are some have their rights were returned eventually. You will see in this document Mr. Speaker, I have mentioned afew examples that the rights of those indigenuous people were eventually restored, we are begging for fairness. We want to enjoy a happiness in this country like everybody else. I thank you, Sir.

**Com. Maranga:** Thank you Hon. Kisiero and mmeona nimempatia nafasi kidogo yeye vile vile alikuwa mheshimiwa kwa hivyo lazima tutambue viongozi wetu, ama namna gani?

**Wote:** Ndio.

**Com. Maranga:** Asante, na nyinyi vile vile ni viongozi msije mkajisahau. Aah, tunaita sasa Checkman Sioi, Checkman ako? Karibu, atafuatiwa na Isaiah Karijoo, Isaiah Karijoo ako?

**Isaiah:** Niko.

**Com. Maranga:** Okay, basi Mzee wewe ndiwe utafuata. Thank you. Checkman, you have three minutes, Sir, give your main points. If you can do it earlier, the better.

**Checkman:** Thank you.

**Com. Maranga:** And Mheshimiwa uwache hiyo memorandum na sisi ...

**Hon. Kisiero:** Iko tayari.

**Com. Maranga:**... na umeandika jina lako.

**Hon. Kisiero:** Yes.

**Com. Maranga:** Thank you, asante.

**kman Sioi:** Mimi naitwa Checkman Sioi, ni mkaaji wa Saboti Division, aah Saboti Constituency pahala panaitwa Kibomet. Eeh, dia yale yawe zungumzwa bali nitataja kuhusu mambo ya Parliament. Wakati tulianza uhuru tulipopata uhuru mwaka wa sitini na likuwa na Bicameral Parliament pamoja na Regional Assembly. Kweli, kulikuwa na wale kile kitu tunaita checks and balances na a in practice kwa sababu Lower House ilikuwa inajadilia bills halafu sasa zinatumwa katika Senate ambayo ilikuwa inachunguza na ebisha mahali inawezekana halafu inapitizwa iwe Law. Walakin ilipovunjwa na Regional Assembly zikavunjwa tukabaki na National nbly peke yake na National Assembly imefanya kazi, ndio, lakini kuna makosa.

muda National Assembly imekuwa kama rubber stamp ya ku-rubber stamp decisions ama intentions ambazo Executive inataka zwe. Kwa hivyo tungependa ningependa ya kwamba turudishe ile mwenendo tulikuwa nayo tulipoanza wakati wa Independence. sasa hata mtaona wale mnasoma magazeti, Parliament imeenda imeunda Public Service Commission yake na mnaona ya kwamba tea yenyewe kwa mishahara yake, kwa masilahi yake. Na unaona kweli hata mshahara sasa umepita kile kiwango kile ambacho tukiongeza mishahara tatu ama nne ya parastatal boss, haitoshelezi. Na haswa hao watu wanaokena ni watu ambao ipendekeza sasa, kwa hivyo tungependa tuwe na another set of decision making body.

kipendekeza mambo ya Senate yaani Upper House, ningependa ya kwamba ile representation katika Senate itoke kutoka kila ct tuwe na representation moja. Yaani katika Districts sasa tuko nazo sabini na moja na ingekuwa afadhali tuwe na hawa sabini na halafu tuwe na nomination kutoka minority communities wale ambao wataketi huko. Katika Parliament, tupatie nafasi minority unities wawe permanently represented, nominated because hawawezi kupata nafasi ya kuchaguliwa tukienda katika Universal ge.

Maranga: Sir, your last point.

erforce: Aah, thank you very much. Jambo la mwisho ni ya kwamba ningependa kuhimiza yale yamesemwa na mwenzangu kuhusu la watu wetu walio Mt. Elgon warudishwe watransfaiwe to be administered in the Rift Valley Province. They should come as a ct. We have appealed for this, our parents have appealed for this in the past in successive Commissions but this has not been ed and I hope that your Commission will favourably look into this request. Thank you very much.

**Maranga:** Thank you very much, asante and may I request you to hand over that small memorandum and register with us.

**erforce:** I think we have one memorandum.

**Maranga:** Isaiah Karjoo, mzee apo halafu atafuatwa na Patrick Etiang. Okay, you will be next.

**n Kapsale Karjoo:** Asante sana mwenyekiti. Mimi kwa majina naitwa Isaiah Kapsale Karjoo. Mimi natoka katika Location ya katika Saboti. Yangu kusema kweli kama vile mzee Khaoya alisema time ni kidogo mambo ya Trans Nzoia ni moto sana na kikana muda mrefu. Nitakuwa brief na nitataja tu kuhusiana na mambo ya squatters. Kusema kweli mambo ya squatters katika Nzoia tungependa katiba iangalie mambo kwa njia hii, kuna squatters ambao waliletwa na Serikali kupanda miti sana sana wengi oka sehemu ya Central. Kuna wengine ambao walikuwa wanafanya kwa mashamba ya wazungu ambao pia ni watu ya hapa nchini a ambao wengine wakati wazungu walienda walipea hao option ya kupewa shamba na wengine wakapewa pesa. Hao wengine ye walipewa pesa wengine walitumia pesa vibaya na wakabakia kuwa squatters, wengine wakauza mashamba yao na wakabakia ters. Kuna pia wale watu ambao wali-importiwa kutoka nchi ya Uganda kama labourers ambao wali-importiwa na Serikali ya ni. Hao watu baada ya sisi kupata uhuru hawakurudi kwao na hao ndio imekuwa matatizo zaidi ambao imefanya Trans Nzoia hii geuza ati ndiyo yao kwa sababu Wasabot walikuwa wamehamishwa hapa na waliona ndio walikuja kunyakua hiyo ardhi.

una wale wengine ambao ni claimants ambao ni Wasabot ambao wanarudi kutoka sehemu ile walikuwa wameenda. Tuseme hii bila ambao wametegwa hapa Trans Nzoia wanajaribu kwa njia yoyote ili kuwazuia wanabandikwa majina kama vile ati Sabaot, ati bei kutoka Uganda ati foreigners kutoka Uganda, hiyo tungependa Katiba itambue kwamba kuna watu walihamishwa kutoka Trans na wakaenda Uganda. Na wakati wanarudi wasije wakabandikwa kwamba ati ni wageni. Hawa ni watu wanatambulikana na na vitambulisho yao wamehangaika, wameenda pande ya Teso wameenda pande ya Busoga na wamerudi wako hapa nyumbani. walienda pande ya West Pokot wamerudi, sasa hapa kama itakuwa Serikali ama kamati hii ya Tume lazima iangalie mambo yao kupea hao makao kutokana na mashamba ya Serikali ile bado iko kwa mkono ya Serikali.

**Maranga:** Point ya mwisho Mzee, umemaliza?

**n:** Bado sijamaliza namaliza.

**Maranga:** Haya, ya mwisho.

**n:** Ya mwisho ningependa kupendekeza kwamba kuwafunga watu kwa ajili ati wamekunywa pombe ya kienyeji sidhani kama ni itu nafikiri irekebishwe. Sababu pombe ya kienyeji kwa wale wanakunywa nafikiri ni halali sababu ndio hata…

**Maranga:** Kwa hivyo unataka pombe ya kienyeji…

**n:** Wale wanataka wakunywe…

**Maranga:** Iruhusiwe kisheria.

**n:** Wafanyie sherehe zao sababu ndio inatumika kwa kimila kwa mambo mengi.

**Maranga:** Ooh. Asante sana Mzee wangu, nakuomba uweke hiyo memorandum yako na uweke sahihi. Thank you very much. is Patrick Etiang. Bwana Etiang atafuatiwa na Christopher Sakwa Sai is it ama Saikwa, Saikwa ako? Uwe tayari.

**ck Etiang':** Kwa majina kamili ni Patrick Etiang' Munyekenye, nina maoni kama yafuatavyo. Wakati nchi hii yetu ya Kenya ilipata , kiongozi wa kwanza alitangaza kupambana na mambo matatu ama magonjwa matatu lakini magonjwa haya matatu hayakamilika ugonjwa ya umasikini. Watu wengi asilimia themanini ni masikini hapa Kenya. Kwa hiyo naomba Tume mpya ambaye inaenda ebisha Katiba mpya iangalie hali ya umasikini Kenya.

upande wa hapa Trans Nzoia, kwetu hapa juu mlimani kuna National Park. Rasilmali hii inasaidia kuleta watalii wengi kuleta pesa Kenya lakini sasa pesa hizi hazisaidii mkaaji wa hapa Trans Nzoia. Tungeliomba Tume, hiyo pesa ingelisaidia kutengeneza ara, kujenga mahospitali hata kuleta moto nguvu za umeme zikuje sehemu hii isaidie Mwana Kenya wa eneo hii.

ali yetu ya Kenya imeajiri watumishi wa Serikali kama vile askari na tunawaita kwamba Watumishi kwa Wote, lakini kazi hii achia watu fulani wameajiriwa na Serikali ya Kenya ambao wanaitwa KPR. Watu hawa wameajiriwa na Serikali, wakapewa mu, wakapewa silaha lakini hawapewi mshahara. Kwa hivyo hawa watu ni hatari kwa usalama wa wananchi hapa.

omba Katiba mpya ambayo inaenda kutungwa ipunguze tupunguze hasa maoni yangu kwamba ipunguze mamlaka ya Rais. Yeye mwenyekiti wa kila kitu nchini Kenya, mkulima namba moja, mwalimu namba moja, mfanyi biashara namba moja, mambo haya olewe.

upande wa ma-Chief, ofisi ya Chief – Ofisi hii inafanya kazi vizuri sana ikisaidiwa na wazee wa mtaa. Nilikuwa naomba kwamba anaji gharama utawala kutoka juu kuanzia kwa Rais mpaka kwa ofisi ya Assistant Chief ama kwa ma-Chief hapa chini iwe mkasa, tukute Chief, tukute D.C na tupate Rais. Lakini mambo ya Assistant Chief, D.O na P.C hawa watu wanapata mshahara ya bure a.

la mwisho ni kwa upande wa uchaguzi, naomba kwamba tuwe na uchaguzi wa kitaifa baada ya miaka mitano, kuchagua Wabunge na Rais wa nchi hii na Rais aongoze kwa kipindi cha miaka mitano, sio miaka kumi au zaidi. Mwisho..

**Maranga**: Thank you very much.

**ck:** Nataka toa ya mwisho tu.

**Maranga:** Okay, toa ya mwisho tu.

**ck:** Ya mwisho naongea juu ya kazi Kenya isiongozwe na Serikali ya Majimbo. Hii italeta ukabila mwingi nchini Kenya na watu yanyasana zaidi. Asante sana.

**Maranga:** Thank you very much, nakuomba utupatie hiyo memorandum yako na uweke sahihi. Christopher Saikwa, aah ita uwe unafika ukiona mwenzetu ama mwenzangu amejaribu kumaliza unakuwa karibu kabisa. Mwingine ni Jonathan Cherogon, Jonathan, you are coming to speak, utakuja kuongea?

**than:** Ndio.

**Maranga:** Okay, sawa. Uwe tayari.

**stopher Khaefa:** Basi Mwenyekiti na halmashauri yako, mimi kwa majina ni Christopher Khaefa, Chief mstaafu. Kwanza sema kwamba watu wameongea juu ya mambo ya Chief, Chief hawezi kupigwa transfer kwa sababu ya kabila yao. Kabila yao mambo yao, desturi yao na mila yao. Walete mtu mwingine pengine hatahiriwi aende mahali watu ya kutahiriwa atafanyaje na hao Kwa hivyo vitu kama hiyo hiyo ni ya kitamaduni, utawala ya kitamaduni hauwezi kutolewa.

i Bwana Mwenyekiti ni kwamba hawa ma-Chiefs hunyanyaswa na ma-D.C. D.C anatoka mahali pengine ana tabia ya nchi yao ka Chief ambaye ako na tabia ya kabila yake akae kama vile watu wao wanakaa. Hiyo kitu ni mbaya zaidi na anaenda kwa baraza ma chief anafutwa as if sio kiongozi wa watu wengine. Hiyo tunaona ni mbaya kabisa, tunataka hiyo mambo ya tawala wa aina hiyo ni kibarbaric sio utawala mzuri.

ema ya tatu ni usalama katika nchi, usalama katika nchi sisi tunazungukwa na nchi ambayo wamekuwa na shida na silaha zinakuja. ka Serikali wawe macho wanyang'anywe hiyo bunduki yote, naona watu wanakufa naona mtu amepigwa na bunduki. Hata Nairobi ewe City ya Kenya ndio mbaya zaidi na watu wanauawa zaidi wale wanabase makabila wengine wale wako huko pengine ni mwana anauawa. Tunaona usalama hapo hapana kuwa mzuri, nataka Serikali na Katiba iwe mzuri.

ka uchaguzi ujao ifanywe chini ya Katiba mpya. Kwa nini watu walie hata hii Katiba ikiandikwa miaka mitatu ijayo, sisi wananchi utafaidika kwa sababu sio yule Mbunge ambaye ako hako, yeye si permanent na kuishi huko, sisi tutatoa yeye na alikuwa anakataa

tiba iandikwe ya nini? Nataka Katiba hii iendelee mpaka ikwishe, uchaguzi yakuja tunafanya na Katiba mpya.

nu ingine kama sisi hapa watu ya Saboti Trans Nzoia, wakati Tume ya Chesoni ilikuja tulikuwa tunataka Saboti Constituency nywe mara mbili. Na hiyo mimi nataka kusema ya kwamba sisi tuko hapa makabila mawili hapa Saboti, Waluhya na Wasabaot. aka tugawanye hiyo constituency iwe mbili, Mbunge mmoja awe Mluhya na Mbunge mmoja awe Msabaot kwa sababu ya haki ya wao. Kwa nini hiyo kitu, hiyo ndiyo inafanya watu kupigana saa yote unasema clashes kwa sababu watu wengine ekanyangwa. Ni miaka ishirini na miaka thelathini na sita sasa kama Mbunge ni Mluhya lakini mambo mengine wakati scheme eanwa ilipeanwa Waluhya peke yake sababu sauti ilikuwa ni yao peke yao, Wasabaot walinyimwa. Ndio tunasema tunataka mwakilishi wa Bunge tukigawanya Saboti halafu shida zetu ziwe zikipelekwa na hawa, hiyo ndiyo daraja yetu na Serikali.

**Maranga:** Ya mwisho kabisa Bwana Chief.

**stopher:** Ya mwisho ningesema ya kwamba sisi hapa katika town ya Kitale tuko na watu tunaita chokoraa na Serikali inaona hawa wakitaabika wakirokota vitu mbaya mbaya saa saa sio Wakenya. Kwa nini hawa watu wasitengewe sehemu waelimishwe kama watoto mpaka watu wa huko ukienda huko town unaona pickpocket wako.

ho, nataka sehemu ya Rais ichukue miaka kumi na kama bado anataka aendelee, kura ya maoni itolewe na wananchi wenyewe. unga wale wenzangu wamesema ya kwamba Wilaya ya Mt. Elgon ikuje Rift Valley. Tuna sababu na iko katika memorandum yo Mheshimiwa Kisiero atawapa. Tuna sababu ya kusema hivyo, tunataka Wilaya ya Mt. Elgon ikuje Rift Valley halafu mambo we sawa sawa. Namaliza Bwana Mwenyekiti hapa…

**Maranga:** Bwana Chief ulikuwa umemaliza lakini maliza.

**stopher:** Ya kwamba mambo ya squatter, mambo ya squatter vile wenzangu wengine wamesema hata Mheshimiwa Khaoya ema mtu kutoka hapo kuwa D.C ndio ameletwa kuja kupata makao. Hakuna D.C amekuja Trans Nzoia akaenda bure bila kupata a na squatter yule yule wanaimba hapana angaliwa. Mtu kutoka hapa sio mtu, ametoka Kisii ametoka huko anakuja pata shamba na hawa watu ya Trans Nzoia wakizaa wataenda Kisii kweli kupata shamba? Mambo ya Trans Nzoia ibaki na wananchi wa Trans peke yao hapana enda kuleta watu wengine. D.C akuje na aende hapana pewa shamba si bado ana shamba, alitoka kwao ini? Ana shamba.

**Maranga:** Okay.

**stopher:** Kwa hivyo tunasema ya kwamba isije ikawa hapa unasema ni ya kabila arobaini na mbili na makabila mengine hapana iko le sehemu ya arobaini na mbili. Watu walifunga kwao wameweka majimbo yao. Nikimaliza nasema nataka Serikali ya Majimbo, sana.

**Maranga:** Haya yule anayefuata ule niliita anaitwa Jonathan Cherogon atafuatwa na Edward, Edward Chepkortit, utaongea?
.

**than Cherogon:** Basi mimi naitwa Jonathan Cherogon kutoka Saboti Location.

**Maranga:** Main points, Sir because time na watu ni wengi.

**than:** Ama kwa kweli mimi sitakuwa na maneno mengi ya kusema isipokuwa tu mimi naunga wenzangu ambao wamesema ya ba tuwe na Majimbo katika Serikali ijayo.

i Bwana Chairman, mimi naunga wenzangu waliosema ya kwamba Mt. Elgon irudi Trans Nzoia na constituency igawanywe mara Mt. Elgon, hivyo hivyo Saboti. Saboti nayo igawanywe mara mbili iwe constituency mbili kwa sababu hii constituency ni kubwa Bwana Chairman.

tu Bwana Chairman sisi tumenyanyaswa sana na wenzetu, Serikali ingekuwa na control price kwa sababu unakuta Wahindi na biashara wengine wanajifanyia bei zao tu. Kwa mfano mbolea, unaweza nunua mbolea leo saa mbili kurudi huko saa sita utakuta bei imekuwa bei ingine kwa wazungu huko. Kwa hivyo Serikali ingekuwa na control price ambayo haiwezi kunyanyasa mkulima.

e Bwana Chairman kuna watu ambao wanaitwa squatters. Wazungu waliandika watu, wazungu wakatoka wakaacha hao watu sisi Waafrika tukachukua hizo mashamba tukazidi kuandika hao watu halafu baadaye tunatupa hao watu nje tu. Hao watu ambao fanya na wazungu na Waafrika badala ya kutupwa nje tu ovyo ovyo huyo landlord awapatie watu kama hawa acre mbili na zaidi ababu wamefanyia kazi kwa muda mrefu.

**Maranga:** Asante sana, umemaliza? Ya mwisho…

**than:** Ya mwisho Bwana Chairman mtu mmoja awe na kazi moja katika Serikali hii kwa sababu kwa mfano, unaweza kuta mtu Makamu wa Rais ni Makamu wa Rais na hali tena ni Waziri katika ofisi fulani. Kwa hivyo hiyo nafasi ingewachia naye hata na ne wafanye hizo kazi.

**Maranga:** Thank you very much, asante Mzee nakuomba uweke sahihi na hiyo memorandum yako utawachie. Edward ortit atafuatwa na Stephen Makari, ako? Stephen, Stephen Makari? You will speak eeh, you are next.

**rd Chepkortit:** Kwa majina ni Edward Chepkortit, ningependa kupendekeza hoja kadhaa kwa hii Tume. Ya kwanza nitaanza wa Katiba mpya napendekeza kwamba the role of Kenyan Police should be re-defined kwa sababu wamekuwa ni watu

nangaisha wananchi instead ya kuwasaidia kwa sababu kazi yao zaidi imekuwa ni kushika pombe na kazi zingine za kulinda usalama ananchi wamewacha. Tunasema kuna mambo ya Bill of Rights, wakati maaskari ama askari wanakuja kushika watu wanaingia ngia wanapekuapekua ilhali Constitution inasema kwamba inatakikana wa-produce search warrant. Hii haifanyiki na endekeza kwamba kuwe na msisitizo kwamba sheria ifuate hao mapolisi ambao wataenda kinyume na sheria. Tena cha pili, jinsi wanashikwa wanashikwa kama wanyama, hiyo pia irekebishwe. Kuna mambo tena wakati mtu anashikwa unaona anawekwa nde ati wanafanya investigation, napendekeza kwamba kama kulingana na depending with the nature of the crime, investigation we kwanza ndio huyu mtu ashikwe. Si ati ashikwe ndio aende rumande ndio wanafanya investigation. Na pia the condition in our an Remand Homes and Prisons please ikuwe re-defined in the Constitution. Watu huko wanakaa sijui ni kama dunia ingine.

, nitakuja kwa minority rights, na nashukuru sana kwa Commission kwa chapter ya Constitution, mumeweka chapter ya Minority s. Ni vizuri sana kwa sababu ninapendekeza kwamba Minority groups wamenyanyaswa sana Kenya, kwa mfano, vitu mbili we political leadership and land rights. Watu hao wamenyimwa kwa sababu za kisiasa na pengine hawana representative in the ment. Hasa hapa Trans Nzoia, Trans Nzoia inajulikana kwamba ni District ama eneo ambalo halina mwenyewe. Trans Nzoia a inayo, Trans Nzoia ina mwenyewe. Msabot alifukuzwa na kwa sababu ya hiyo napendekeza kwamba the colonial land ances zitolewe na waseme kwamba wale waliokuwa wanakaa hapa wapewe, we have Government land, we have A.D.C farms, saa y are not operational. I suggest that Sabot people who are still landless should be given these lands na inatakikana iandikwe kwa itution kwamba we have the evidence, we have all the necessary documents na tena napendekeza hivi…

**Maranga:** Ya mwisho.

**rd:** Ya mwisho, kuna pendekezo ambayo ilikuwa inasema kwamba kukuwe na ninety constituencies in Kenya kwa sababu under rity Rights nasuggest kwamba under Trans Nzoia kukue na special constituency ya Wasabot ili nao wakue na sauti Parliament. e. May God bless Kenya.

**Maranga:** Okay, next.

**hen Makari:** My names are Stephen Makari, I have come here on behalf of the Catholic Diocese of Kitale, Justice and Peace. ave got a document we want to present, a memorandum but I would like to also…

**Maranga:** Give us the main points, Sir.

**hen:** Yeah.

**Maranga:** Yeah.

**nen:** So, I want to talk about land, I wanted to re-emphasize the fact that because of land problems, we propose that the power or thority to give land, any land in this country especially in this Constituency should be removed from the Office of the President. ndio unaona ma-D.C na wengine wanapata mashamba kwa sababu wako katika order ya Office of the President. Pia tuna hii ya watu kuchukua shamba ambayo tunaita Public Land. Tungependa all public land ijulikane na ipewe L/R numbers ili tujue shamba public land ili mtu asijaribu pengine kulichukua. Jambo lingine, public land inatusaidia sana kwa mfano tuna shamba kama hii Kefis na KARI land na Prison land inasaidia sana nchi hii kwa mambo ya research na mambo kama hayo. Sasa ikiwa watu ambao ependa kupata mashamba watachukua shamba ya Kenya Agricultural sijui station, Institute watachukua shamba kama hii ya Kenya Health and Inspection Unit ni shamba la Prison, utaona ya kwamba mwishowe hatutakuwa na shamba lolote ambalo litafaidi watu kijumla, tungependa mashamba kama hayo wenye wamepewa ikiwezekana Tume hii iwezeshe hiyo mashamba kupokonywa tena ishiwa public.

mbo lingine ningependa kusema wengi wamesema juu ya mambo ya squatters, ningependa kusema hivi Bwana Commissioner man, sio vizuri baada ya miaka ya uhuru muda mrefu sana watu fulani wakiitwa masquatters. Unajua squatter ni mtu mwenye ame aa vizuri, hatupendi kuona mtu ya kwamba ameitwa squatter. Hatuwezi kupenda wakati wa independence huu mtu aseme huyu ni ya halisi, huyu ni squatter. Lazima tuwe na mechanism katika Constitution ambayo itawaruhusu Wakenya wawe na uhuru na wawe vaseme ya kwamba nimekaa vizuri, sio kusema ati mimi squatter. That one…

**Maranga:** Una unapendekeza nini?

**nen:** Napendekeza ya kwamba vile mmoja alisema hapa kuwe na situation kama kwa mfano mtu kusema ya kwamba kukosa ba ndiyo kuwa squatter, lazima Constitution ya Kenya iguarantee means juu ya mtu huyo kuishi vizuri na ajione ya kwamba awe na ba ama asiwe na shamba ako vizuri. Infact sio kila Mkenya lazima apate shamba lakini lazima mtu apewe ile social mechanism yo itamwezesha kukaa vizuri. Ningependa kusema ya kwamba pia kama kuna mtu yeyote tuna squatter upande mmoja na upande gine tuna ile inaitwa land grabbers. If there is anybody who got land in a way which is not fair, huyo mtu lazima hiyo shamba tumpe muda mfupi pengine six months ili shamba hiyo awe ametoka. Ningependa kushukuru sana His Excellency wakati alijaribu lolea wale watu ambao walikuwa wamepata shamba ya Kitalale kwa njia ambayo haikuwa halali. Kwa hivyo unaona ya kwamba makosa katika upande wa kupata haya mashamba.

**Maranga:** Last point.

**nen:** Last point ningependa kusema ya kwamba tuwe na kitu kama Truth and Justice Commission ambayo itaangalia wale watu o wana shida ya mashamba, sio watu kujaribu tu kusema tungepata shamba njia ambayo iko haphazard. Tuwe na kitu institution ya nguza mambo hayo na mambo hayo pia ishirikishe wale watu ambao pengine kwa njia moja ama nyingine waliweza kuumia kwa bo ambaye ilikuwa inaitwa land clashes. Hawa watu lazima ikiwezekana wachunguzwe na hiyo Commission.

ependa kuzungumzia pia jambo lingine la general issue on land. Ningependa kuzungumza ya kwamba shamba kubwa kubwa hizi he ningependa pia kupendekeza the upper ceiling ya shamba iwe 200 acres. Pia ningependa kusema ya kwamba ile idle land lazima xed. Mwisho ningependa kusema ya kwamba hili jambo la Trust Land hiyo iondolewe ili tuwe na kitu ambayo inaitwa Registered unity Land. Hiyo itaangaliwa na watu wenyeji wenye shamba hilo wataangalia vizuri kuliko kuwa na general issue ya kusema Trust Na wale Trustees pia ndio hao wajaribu kupokonya hiyo shamba.

u upande mwingine, natural resources ningependa kuunga watu ambao walikuwa wamesema ya kwamba 20% or so ya products ba kwa hiyo natural resource kama hii National Park and whatever ifaidishe watu wa hapa. Kama ni shule isaidie kuendeza hiyo na bo ingine ya welfare ya watu.

**Maranga:** Thank you very much.

**en:** Thank you very much, ningependa pia kumalizia kusema ya kwamba…

**Maranga:** No, ongojea kidogo utaulizwa swali.

**en:** Yes.

**Mosonik:** Ukasema authority ya kupeana ardhi itolewe kwa afisi ya Rais lakini hukufanya pendekezo iwekwe wapi?

**en:** Yeah, nilikuwa nataka kupendekeza all the land in a particular area hiyo land iwe under the Local Authorities, tuwe na wazee Local Authorities majorly napendekeza ambao wako elected. Hao wakae na waone nani wanastahili kupata shamba, hivi eana on merits of need for that land but if it is in the Office of the President, tunapata hiyo abuse ambayo tunazungumzia.

**Maranga:** Thank you very much Bwana Makari but I can see you have a number of your people here, do they really want to because you have presented their memorandum? And are they going to speak?

**en:** Yeah.

**Maranga:** Because I have got Patrick Busolo, Mary Nyambane, Shadrack Koech, Lorna Karani, Silas Juma, Boniface oike. Do you want all of you to speak?

**ker:** Yes, on different topics.

**Maranga:** Alright, then I will give, I will be more, Okay proceed.

**alwa Patrick:** Majina yangu ni Wamalwa Busolo Patrick,

**ence**: Bwana Commissioner, mimi nime-specify Saboti. Wenye walifukuzwa na wazungu pekee yake.

**Maranga**: Lakini kuna Wasaboti ambao ni Waganda?

**ence**: Hawako. Walioko Uganda ni Wasebei.

**Maranga**: Okay thank you, next point.

**ence:** Next point ni kuhusu mambo ya local authority na upande wa MPs. Ningependekeza Bwana Commissioner, kama cillor anaenda kuchaguliwa awe form four and above. Mbunge awe diploma holder and above. Kwa sababu, pia hiyo ni kazi na penda watoto wetu ambao wamesoma pia wapate hiyo kazi.

wisho, ni kuhusu mambo ya korti. Ningependekeza cases za nchi yetu, ingawanywe katika sehemu mbili. Cases kama robbery with ce, murder na rape, zifanywe katika locals. Na cases kidogo kama, theft, kupigana, land disputes, mambo ya dowry korti iundwe bani, ambako cases kama hizo zitafanywa na wazee nyumbani.

mwisho, kwa upande wa polisi arrest, ningependekeza hivi, kabla ya polisi kushika mtu, ningependekeza wakuje nyumbani waulize wa mtaa kabla mtu hajashikwa. Kwa sababu wengi huwa wanashika watu na kwenda kuwapiga.

**Maranga**: Thank you very much, weka sahihi, asante kwa maoni yako. Wananchi wakati tunauliza mtu ni kutaka kujua kabisa namaanisha nini. Kwa sababu mtu anaweza akamaanisha kitu fulani na anamaanisha kingine. Kwa hivyo ndio sababu tunauliza ndio na uhakika. Anayemfuata ni Peter Ndirangu. Hayuko. Stephania Kalama. Okay kuja, huyu atafuatwa na Benard Mumari. d Mumari ako? Hayuko. Do we hava Masika Christopher. Utaongea? Kuwa karibu hapa sasa.

**ania Kalama**: Majina yangu ni Zaphania Kalama, natoka katika Saboti division. Langu Bwana Commissioner, ningetaka kusema tika utangulizi, Katiba ilioko wakati huu haina utangulizi wa Kenya ambayo inastahili kusema ya kwamba Mkenya ameamua mambo hivi hivi, kwa hivyo Katiba ya saa hii, haisemi hivyo. Kwa hivyo ningependa Katiba ya sasa, kiongozi wa taifa akiongea, aongee na Wakenya wenzangu. Ndio iwe utangulizi wa Katiba.

de wa administration. Ningependa kuanzia upande wa Mukasa, Mukasa ningependa achaguliwe na wananchi. Asiwe appointed, sababu anafanya kazi ya wananchi. Upande wa chief. Chief na councillor wako katika location moja na wanafanya kazi moja. etaka councillor awe mwenyekiti, chief awe kama mwandishi ili arahizishe kazi, watu wasing'ang'anie madaraka. Na uamuzi wa nchi katika upande wa mtu mmoja. Tuseme kama sasa, President akikosana na President wa Uganda, anaweza kuamua wapigane. i tungetaka uamuzi uwe katika mikono kama ya Mawaziri ambapo kukiwa na shida fulani anaitisha baraza la Mawaziri wanaongea jambo kama hilo.

**Maranga**: Na akikataa kuitisha na yeye ndiye mkubwa?

**ania:** Ndio tunataka kupunguza hayo madaraka, yatoke kwake. Halafu nyingine, upande wa education na matibabu ningependa na hivi. Ukiangalia katika budget ya juzi, Serikali imetoa pesa tu katika Kenya. Kwa hivyo ningependa upande wa elimu iwe free, abu iwe free na upande wa harambee iwe abolished, kwa sababu tuko na pesa ya kutosha. Ni sababu ya Serikali haipangi njia ya ia hizo pesa.

**Maranga**: Asante Mzee wangu, thank you. Okay next. Masika Christopher.

**ka Christopher**: Majina yangu ni Christopher Masika nina haya. Serikali zaidi sana ichunguze kusaidia maisha ya mkulima, haswa e maneno ya soko huru. Tumekuwa tukinyanyaswa sana. Pili, administration ianzie kwa Mkasa, chief atolewe, DO akuweko, DC eko, from the DC direct to Permanent Secretary. Powers za President zikuwe reduced kwa kuchagua Vice President na hata ney General. Kwa upande wa matibabu, ningependa maoni yangu ni kwamba watoto chini ya miaka sita na watu wazee above 55 wawe wakipewa huduma ya bure. Kwa upande wa President ningeomba kamba ingekubalika pia naye awe akihudhuria Bunge kila kikao, ndio ninasema mamlaka yake yapunguzwe.

ho kura ipigwe kufikia mahali Katiba imetengenezwa ama imefikia. Kwa sababu maoni yangu ni kwamba ningependa kuwe na nent commission ya kutengeneza Constitution. Asante Mungu awabariki.

**Maranga**: Asante, next tunaita Samson Musera (Pastor). Karibu, you have a minute. Then atafuatwa na Isaak Eluk. Isaak ako? uko. Do we have Musa Kibet? Wycliff Simiyu? Charles Ilimo? Utaongea? Okay. Anza kwa majina yako, one minute.

**on Mwangi Musera**: Kwa majina naitwa Pastor Samson Mwangi Musera. Ninahudumu katika kanisa la PAG, hapa Kapretwa. zungumzia kuhusu Katiba yetu ya Kenya. Katiba ni asante kwa wale ambao walifikiria wakasema tuwe na Katiba mpya na watu vatoe maoni. Alikuwa na kusudi sawa sawa. Maana tukiangalia kwa Katiba ambayo tunatumia sasa, huenda ilitengenezwa na mtu a na ndio inatutatiza. Mimi kwa maoni yangu ningependa kusema hivi. Mimi ni mchungaji ninachunga watu, ama ninahudumia watu di. Na mtu akihudumia kikundi, lazima awe chini ya kikundi kile, sio wewe uwe juu ya kikundi. Rais anafaa awe na mamlaka yo inamfaa ajue kwamba anahudumia wananchi.

**Maranga**: Pastor, ningetaka wewe unipatie mapendekezo.

**r Samson**: Pendekezo langu ninasema, mamlaka ya Rais yapunguzwe.

**Maranga**: Okay, that's all, next?

**r Samson**: La pili, ningependa hivi, mwenzangu mmoja alizungumza hapa na mimi mapendekezo yangu yanasema hivi. Kweli tuna o, tunazaa, tunalinda, tunalea. Mtoto ametoka hapa kijana ameenda ng'ambo ametoka huko na mke. Atakuja kwa maisha ya bani kwangu. Na msichana ameenda kule amezaa mtoto anakuja naye. Halafu mwingine akasema basi amekuwa ni mali yako. na yule mtoto anamzazi wake ambaye anatakikana amshughulikie.

**Maranga**: Pastor ya mwisho. Sitaki unielezee, kwa sababu naelewa vile unaeleza. Kama unasema kuhusu citizenship, utuambie, unataka msichana na kijana wapate haki sawa. Useme.

**r Samson**: Mimi ningesema hivi, kijana ni kijana anaishi pale nyumbani. Msichana akizaa mtoto apewe mzazi wake ili amulinde.

**Maranga**: Yaani yeye msichana sio mzazi?

**r Samson**: Msichana ni mzazi na akija kwangu sasa ataleta mzigo mwingine juu ya mzigo mwingine. Sasa mimi ningependa hivi, wa mtoto kijana ajulikane ili to share kulinda mtoto huyu.

**Maranga**: Na kama huyu kijana hana mzazi wake?

**r Samson**: Msichana hawezi kuzaa na mti, lazima azae na mtu.

**Maranga**: Mimi nimekubali hivi, umesema kijana amezaa na msichana. Si ni hivyo? Na mtoto amepatikana. Sasa wewe ma huyu mtoto amepatikana arudishwe kwa mzazi wa kijana. Si ndivyo umesema.

**r Samson**: Nasema kijana achukue mtoto wake, ni hivyo nilikuwa namaanisha.

**Maranga**: Na nikauliza yeye pekee yake alee mtoto?

**r Samson**: Ukienda kutafuta kazi si utafanya kazi yako.

**Maranga**: Okay.

**r Samson**: Mwisho, ningemaliza hivi, mambo ya urithi.

**Maranga**: Na hiyo ndio sentence ya mwisho.

**r Samson**: Mambo ya urithi, watu wamesema lazima mzee na mama tuwe sawa. Lakini sehemu moja itatusumbua kwa Katiba utakubali namna hiyo. Mimi pendekezo langu linasema hivi. Mke akishaolewa ni mke wa mzee nyumbani. Na mali ile ya mzee mke kusaidiana maana Mungu wakati aliumba Adam, alimpa mke Hawa akamwambia, wasaidiane.

**Maranga**: Mzee sema pendekezo?

**r Samson**: Pendekezo langu nasema hivi, urithi ulindwe na mzee.

**Maranga**: Asante, enda hapa uweke sahihi. Next Charles Ilimo. Charles Ilimo atafuatwa na Joash Murunga. Ako? Joash you ere? Okay you will follow. Do we have Nelly Lawendi? Okay, utafuata.

**les Ilimo**: Kwa majina, ni Charles Ilimo, kama ilivyotajwa.

**Maranga**: Sema vizuri, sema kwa microphone.

**les.** Natoka katika Kiminini division, na maoni yangu ni kwamba, kama wengi wamenena kuhusu mambo ya ugawaji wa ardhi na taka kusema ya kwamba kwa mambo ya ardhi wengi wamekuwa wakizungumzia kwa mambo ya ufisadi. Kwa hivyo ningependa na ya kwamba, kuhusu mambo ya ardhi kuna sehemu ambayo Serikali itafikiria kumpa squatter. Kwa hivyo hayo mambo ningeona vamba, Tume ingechukuliwa kutoka kwa sub-location mpaka division ili kukikisha ya kwamba, huyu mwenye anapewa ardhi hiyo hana chochote. Pendekezo langu la pili, kuhusu mambo ya hosipitali ambayo Serikali ilisema ya kwamba, yaani watu wagawane na. Lakini, kwa wakati huu unapoenda katika hospitali ya Serikali ama yetu ya wilaya unaambiwa kila kitu wewe uweze aramia.

**Maranga**: Unapendekeza nini?

**les**: Pendekezo langu ni kwamba katika wale ambao wanasimamia mambo ya hosipitali pia tuwe na mwakilishi katika watu jiweza kutoka katika location. La kumalizia, kuhusu upande wa Waturkana, haswa mimi ni Mturkana kuna watu hapo awali ilikuwa amba unaweza kutoa mahari lakini kama hautaweza kumalizia, ama hautaweza kuwa ndume, basi wale watoto hawataweza abiwa ni wako, wala hata huyo mke hatahesabiwa ni wako. Ningependa katika kurekebisha Katiba wakati huu hilo jambo guzwe.

**Maranga**: Unataka tuwambie Waturkana wasikatae maneno?

**les:** Ndio, iwapo kama umetoa mahari na hali haujaua yule ndume, wale watoto ikiwa unawalinda vizuri, wale watoto wabaki ni .

**Maranga**: Thank you very much register with us.

**les:** Kumalizia tu, kuna wale wasichana ambao wanapewa mimba, na mtu anaruka huyo msichana hataweza kuoa. Kuna mila yo ilikuwa ikiendelea hapo awali, ambayo ilikuwa ni kwamba mtu anaweza kulipa fine ambayo alikuwa akipewa. Kwa hivyo iza na hiyo iendelee. Asante.

**Maranga**: Thank you very much, next Bwana Joash Murunga. I want you to be to the point. We have so many people. We over 60 people to go through.

**Murunga**: Asante sana kwa Tume ya Kurekebisha Katiba. Yangu ni Joash Nyongesa Murunga. Hayo ndio majina yangu. ni mwalimu Saboti Secondary School. Nina maoni kuhusu election. Naona kwamba Electoral Commission iwe empowered, ili ba iwe iki-set date za general elections, ambazo haziwezi kutumiwa kama kikwazo kwa vyama vingine. Namba mbili, provincial istration isiwe ikihusika katika mambo ya elections. Kwa sababu tunaona kwamba kuna corruption nyingi ambazo zinaweza kuwa okea kama vile miaka iliyopita. Provincial administration isihusike katika mambo ya elections. Tatu, Minister wa Education asiwe a kutoa policy kuhusu haswa discipline ya wanafunzi shuleni ila anatakiwa kwamba ajihusishe na waalimu ambao ndio wako chini, o wanaweza kuwa wanajua mengi kuhusu discipline ya watoto.

policy ya discipline lazima irudishwe kwa waalimu wazungumze na wazazi wenyewe ili kwamba wajue wanafunzi wanaweza kuwa lined namna gani. Promotion of teachers. Vile ishakuwa in the past, tumeona kwamba waalimu hawakuwa wakiwa promoted Kwa sababu unaona kwamba promotions zilikuwa zikiendeshwa kwa njia isiyofaa. Napendekeza kwamba mwalimu yule yeyote ye yuko trained akimaliza miaka mitatu katika service bila kukatizwa apewe cheo kingine ambacho kinafuata ama grade nyingine

yo inafuata.

**Maranga**: Your last point Sir?

**n:** My last point, ni kuhusu 85% of form one intake. Tumeona kwamba hii imefanya, hii exercise kuwa so much localized, ili nba wanafunzi hawajui Kenya yao. Kwa sababu wale ambao wanachukuliwa form one, kutoka kiwango kama cha district, takiwa kwamba nao wapate nafasi waende katika shule zingine za province ili kwamba waweze kujua Kenya yao. Wale ambao chukuliwa katika province wawe wakichukuliwa province za kupelekwa mahali popote katika nchi ya Kenya. Kwa national ls, provincial school ili kwamba tuwahi kuwa na Kenya moja. Wanafunzi watuajua zaidi Kenya yao. Asante.

**Maranga**: Thank you very much, and please give us that memorandum and sign our official register. Nelly una dakika moja. Na ia Nelly, tuta-reduce iwe nusu dakika ndio watu watoe ile point haijazungumzwa hapa.

**Lawendi**: Kwa majina naitwa Nelly Lawendi. Maoni yangu, ni kuhusu haki ya akina mama na watoto wasichana. Kwa mambo ajisi. Mimi natoa maoni ya kwamba wale wanaume ambao wananajisi akina mama na watoto wasichana wangepewa adhabu ya Hao watu wangeuwawa tangu zamani haya mambo yangekuwa yamekwisha. Kwa sababu baba hata anaweza kumrudia mtoto na yeye ndiye aliyemzaa.

**i**, ni kuhusu mambo ya title deed. Mama apewe pamoja na mzee. Iwapo mzee ana wanawake wawili ama tatu kila mmoja apewe eed yake ili mama awe na haki yake sio kunyanyaswa. Yangu ni hayo tu.

**Maranga**: Asante mama. I want people to be brief like mama Nelly. Paul Eseme. Mike Muose. Less than a minute. Then we Patrick Lukosi. Hayuko. Protas Wafula. So we have Mike Muose. Sema majina.

**Muose**: Jina langu ni Mike Muose. Ningependa kutoa mapendekezo yangu kadha wa kadha.

**Maranga**: Hapana, machache tu.

**:** First of all, I would like to base on political parties. They should be given funds to support their parties. Second thing is that, hould maintain discipline and co-operation. Another thing is that, whenever he goes astray, he needs to be impeached. Another on the side of defence, it is very important to have security in the country. Without security I think we might have no economy. So nacy must put forward rather than violence, becaue if you use violence you will not build anything. So what is very import ant is is very important.

**Maranga**: Your last point?

Muosi: Another thing, education must be put forward and to see that anybody who is having knowledge should not go astray. He now what he is doing. Lastly is that I need Federal Government. Federal Government must be practiced. Another thing is on the f land policy. There are some communities that made an agreement with Europeans, to be given back their land. For example, ai and Saboti and they were not given funds. And with me I am appealing to the Government if they are not going to give us our we are going to deal with British rule and get our lands.

**Maranga**: Next is Kiraba John. You have less than a minute to give me the main points. Eliud Masinde you will follow next.

**a Wanjala John**: Kwa majina naitwa Kiraba Wanjala John kutoka Machewa. Ningependekeza ya kwamba Wabunge na ziri, mishahara yao ipunguzwe, ili iwasaidie watoto wanaorandaranda mijini. Kila wilaya iwe na shule ya kurekebishia tabia na o mengine. La pili, wahalifu sugu, wakithibitishwa zaidi ya mara tatu kortini kwa makosa inatakikana wafungwe maisha. La tatu, ang'anyi wezi kwa vituo vya magari, husababishwa na hao manamba. Kwa hivyo hao manamba inatakikana waondolewe katika vya magari.

wisho KGGCU na KFA vinatakikana viongozwe na Serikali ili wakulima waweze kuimarisha kilimo kwa sababu kilimo ndio uti wa ni.

**Maranga**: Thank you very much, Eliud Masinde, atafuatiwa na Winrose Kiruim ako? Hayuko. Emanuel Mutoro, you will be

**Masinde**: I am Eliud Masinde. 8.4.4. system should be abolished and introduce new system which is 7.6.3. And Headteachers d not stay in a school for more than five years. If a chief is from tribe 'A' the assistant should be from tribe 'B' not one tribe. MPs d not be for more than two terms. Employment opportunities should be given according to tribe ratios.

ose that the Office of the President should be removed from the Constitution because it is being done through tribalism.

**Maranga**: Thank you very much, your last point.

: That's all.

**Maranga**: Thank you very much, please sign our register. And give your memorandum. The next is Emmanuel Mutoro. atiwa na Moses Kemboi, do we have Moses Kemboi, we do not have him? Dancan Masindi. Then we have Japheth Wanyonyi. ko. John Sitati. Hayuko, Erick Koroti. Hayuko. So Emmanuel Mutoro proceed.

**anuel Mutoro:** My names are Emmanuel Mutoro Watitwa.

**Maranga**: I can see you have a memorandum, just give us some few points. One minute.

**anuel**: Power, the people and the Constitution. I think the Constitution should be available in all mother tongues spoken in the ry. The Executive. Proper and clear picture of separation of powers between the Executive and Legislature should be there. , Parliament and election, the President should not be an MP. Lastly, those people owning large scale farms should be reduced 100 acreas. Thank you I think that's all.

**Maranga**: Thank you so much. Alex, I think Alex Kimasweti aliongea, Pastor, I think he talked. Humphreyk Ndiwa. Rev. n Cheloget. Wetili Mukwaya. Karibu Mzee.

**i Mukwaya**: Speaker iko wapi? Wacha nijaribu kwanza. Naheshimu Tume ya leo. Naheshimu mkubwa wa Kenya Rais Moi, ababu asingalikuwa yeye hawezi kuwa hapa.

**Maranga**: Sema jina Mzee na una dakika moja.

**i Mukwaya**: Mimi jina langu naitwa Wetili Mukwaya natoka Kimini ni shamba la matunda. Maoni yangu, machifu wakuwe ngo. Chifu wakuwe kwa mlolongo kwa maana yeye haendi transfer. Maoni mengine, inatakiwa wakubwa na mdogo wakuwe kwa sababu niseme hivyo, mkubwa anaweza kukosea mdogo anawekwa ndani na mkubwa ukipeleka report hawekwi ndani. sheria haitakiwi. Ya mwisho kuoa: sisi tunaoa mwanamke, mwanamke analipwa ng'ombe kumi na tatu na mbuzi. Na hiyo ndio e mwanamke wako kuliko mwanamke kukushtaki kortini ati muwachane. Muwachane namna gani?

**Maranga**: Kwa hivyo, unapendekeza namna gani? Kwa hivyo hakuna aja ya kuwachana?

**i**: Hakuna mwanamke kunishtaki tuwachane na mimi nishalipa ng'ombe wangu kumi na tatu.

**Maranga**: Mzee wangu nashukuru kwa kufika mbele ya Tume. Kwa hivyo patia mwingine nafasi usikie maoni.

**i**: Sasa nilikuja kama nimechelewa lakini, Jumatatu nitakuwa huko, Kitale tukiwa na Bwana Khaoya, yangu ni hayo.

**Maranga**: Ngania Sisimua. Next. We have Elisha Senily. Hayuko. Do we have Judith Wasike? Hayuko. Do we have anuel Ndhiwa? Not there. Shadrack Tindi okay you will be next. Uwe karibu hapo.

**nia Michael Sisimua**: My names are Ng'ania Michael Sisimua. One, the President should not be a Member of Parliament. Two,

should be free and compulsory education upto university level. Three, civic, Parliamentary and Presidential election to be conducted fferent days and votes be counted at polling station. Four, there should be no defections or parties crossing the floor. Five, rnment to subsidize farming. Six, Chief Justice should be in charge of Executive powers during Presidential elections.

her one, very important. There should be pension for every Kenyan citizen. Finally, there should be Regional Government. Thank ery much.

**Maranga**: Thank you very much, sign up and give us your memorandum Shadrack Tindi, please be very brief, less than a minute.

**rack Tindi**: Kwa majina ni Shadrack Mamati Tindi. Mapendekezo yangu ni haya. Tangu Kenya ianze vyama vingi, napendekeza li iwe ya mseto na Majimbo ifutiliwe mbali. Jambo la pili, ni kwamba starehe, napendekeza pombe ya kienyeji, yaani "kamalwa" shwe. Starehe, kwa sababu tunaona kwamba matajiri ndio wana starehe kwa kuweza kubudurika na mambo ya beer na wale eji masikini hawawezi kujimudu. Jambo la tatu, ni kwamba sababu Katiba imefichwa, kwa sababu hata wengi hatujaona Katiba ya ni. Napendekeza kwamba yeyote anayeenda kupata kutambulisho, awe akipewa nakala ya Katiba ili aweze kuelewa Kenya yake a wapi inaelekea wapi. Jambo la nne, ni kwamba Rais, PC, DC, DO na idara zingine za kiserikali ziweze kupatiwa asilimia fulani yo inaweza kutumika.

**Maranga**: Your last point.

**rack**: Kwa sababu Kenya tunalia mambo ya uchumi ilhali tunaona Rais ana ziara nyingi zaidi. Jambo la mwisho kabisa ni kwamba kosa limetokea kiserikali wawache kuchagua kamati ambayo inshughulika, bali CID ambao wanahusika waweze kushughulika na iyo ili tuweze kupunguza mambo ya gharama. Asanteni.

**Maranga**: Thank you , hand over your memorandum and sign our official register. Franklin Malaba. Please less than a minute. will be Paul Wanyama. Do have Paul Wanyama? Do we have James Karinyo. Yuko wapi? Utaongea? Basi uwe karibu.

**kline Malaba**: Majina yangu kamili ni Franklin Malaba. Pendekezo langu la kwanza ni kwamba, Madiwani wateule na Wabunge, nafasi ipewe walemavu na wanawake. Pendekezo lingine ni kwamba, gari lolote likipata ajali mahali popote, gari litakalokuja diately after that one, ichukue wale watu wameadhirika wakati huo, wapelekwe hosipitali iwe ya Serikali ama ya kibinafsi bila abu. Pendekezo lingine ni kwamba Wakasa wapewe mshahara kiasi kwamba ili wafanye huduma ya kuchunga ile hali ya kumaliza children. Kwa sababu Wakasa pamoja na chifu wanaelewa vizuri wale watoto wametoka familia gani na ni mtoto gani amekosa a wapi. Sasa wakipewa mshahara na wapewe hilo jukumu watachunga watoto na tuta-eradicate hao street children.

**Maranga**: Your last point.

**kline**: Point yangu ya mwisho ni kwamba, mshahara kwa sehemu kama NSSF ama watu wowote wameajiriwa na mtu mmoja hara wao uangaliwe na watu wa Serikali na hiyo huduma ikuje karibu mpaka sehemu ya division ili kuangalia mambo ya mshahara ntu yule anamfanyia hata mtu kibinafsi, kwa sababu hiyo sheria inasema kwamba hata aandikishwe hata ikiwa zaidi ya watu watano.

**Maranga**: Thank you very much. James Korinyao, next atafuatwa na William Wekesa. Utaongea. Okay.

**s Korinyao**: Mimi kwa majina ni James Korinyao. Pendekezo langu ni sisi kama kabila ndogo katika Trans Nzoia, ambaye kama napatikana kama Turkana. Inasemakama Trans Nzoia ni sehemu za kabila zote. Ningependa sisi tutengewe sehemu fulani katika zote za Serikali ambazo zitaandikwa katika Trans Nzoia hii.

**Maranga**: Kwa hivyo unasema Waturkana wapewe sehemu yao.

**s:** Ndio. Ili wapate siri ya Serikali.

**Maranga**: Lingine na la mwisho.

**s:** Ya mwisho ni sisi tukiwa Trans Nzoia hii, hatuna shamba hata moja. Tunataka sisi nasi tupewe shamba kama wengine. Ni u, Mungu awabariki.

**Maranga**: Okay, thank you. William Wekesa. Atafuatwa na William Kututu. Yuko wapi? Utaongea? Okay.

**m Wekesa**: Mimi kwa majina naitwa William Wekesa. Mimi ni mkaaji wa Saboti. Pendekezo langu la kwanza, ningetaka sheria e kwa kiongozi yule atakayekuwako kama Rais, awe akipatikana na makosa yoyote, sheria iundwe ashtakiwe.

**Maranga**: Next point?

**m**: Ningependa sheria iundwe ambayo inalinda wazee wakongwe ambao wanateseka zaidi katika nchi ya Kenya. Nataka we marupurupu kidogo ambayo inaweza kuwafanya waishi tena miaka kidogo inayokuja.

**Maranga**: Thank you very much.

**m:** Wacha niongeze moja. Pendekezo lingine ningetaka sheria iundwe, kwa sababu tangu Kenya ipate uhuru wale masquatter o walikuwa wanafanyia wazungu na wamenyang'anywa na matajiri ambao walirudia kwa yale mashamba,

**Maranga**: Unapendekeza nini Mzee?

**am**: Sheria iundwe ya kutoa hao watu watoke kwa mashamba ya squatter.

**Maranga**: Thank you very much, next William.

**am Kotut**: Mimi ni William Kotut Naibei. Mimi natoka Kinyoro location. Ya kwanza.

**Maranga**: Order please, mpatie yeye nafasi atoe maoni yake.

**am:** Wagombea viti tunataka waje nyumbani waonane na wananchi ndio waanze kazi yao. Ya pili, tunataka wale wako karibu i, wale watu wanajiita brokers hao ndio wanaumiza wananchi sana. Kama wewe hauna pesa, hakuna chochote utakachofanyiwa. ne, kuanzia kwa Rais, Rais apate kazi kidogo. Msiweke mzigo kubwa kwa sababu atasahau mambo mengine. Mwisho, tunataka fu wawe na wazee wa mtaa pamoja. Thank you very much.

**Maranga**: Next tunauliza Patrick Butek, Patrick hayuko. Do we have T.K. Chumo? Hayuko. Walter Otong, ni wewe? Next ve Gabriel Namasaka. Nani huyo, Mzee unaitwa? Anaitwa nani? Okay, Walter Atong. Just a minute, Gabriel Namasaka ako? ko. Ruth Kweyu, hayuko. Okay Walter, anza kwa majina yako kamili.

**er Otong**: Asante sana kwa Mwenyezi Mungu kutusaidia sisi kufika hapa. Jina langu naitwa Walter Etiang' Otong'. Mimi nasema, za, sisi tunakaa hapa Trans Nzoia, hata mimi nimekuwa mzee kutoka mwaka elfu moja na mia tisa.

**Maranga**: Weka kipaza sauti chini kidogo. Hapo hivyo.

**er**: Kutokea hapo mpaka saa hii, mimi bado sijapata makao kidogo.

**Maranga**: Unataka nini?

**er**: Nataka Serikali itusaidie sisi wengine wale ambao tuko juu ya miti waeke ngazi kwa miti hiyo tushuke chini sisi wote tunyakue da ya Kenya. Sisi tuko vibaya sana. Matajiri ambao mnasema hivi sisi tuko na njaa ile ya kuua. Kwa sababu udogo ndio chakula tu.

**Maranga**: Okay asante. Ya mwisho?

**er:** Ya mwisho mimi nasema nyinyi ambao mnafanya hii Katiba, Katiba hii mimi bado sijaielewa vizuri. Sasa leo ndio mimi nataka

ye hii Katiba vile ambavyo inaendelea, tusaidie sisi tushuke chini tukule matunda ya Kenya. Hakuna maneno mengine. Asante.

**Maranga**: Asante Mzee enda uweke sahihi. Nataka kukwambia Katiba ndio sheria kuu ya nchi. Hiyo ndio maana ya Katiba. a sahihi hapo. Anayefuata ni Kipkalya Namaswa, huyo aliongea. Lawrence Kipsoi, aliongea. Suleiman Kurui. Hayuko. Maunda u. Teresa Chematasi. Haya Karibu. Atafuatwa na Reinson Wekesa. Utaongea? Okay.

**sa Chematasi**: Asanteni, kwa majina ni Teresa Chematasi, mimi ni Msaboti ama mtu wa Elgon Maasai, ingawaje wanasema ni sometimes lakini hapana. Mimi kwa maoni yangu nasema ya kwamba Majimbo iendelee. Ya pili, nastahili sana wakasa na chief delee kwa sababu wako na kazi nyingi sana. Ya tatu, sisi akina mama wajane tunaumia sana, kama tuko na shamba na mzee ufa watoto wangoe wanakusumbua sana. Hiyo inastahili ichukuliwe hatua. Nimemaliza.

**Maranga**: Asante mama na uweke sahihi kitabu chetu rasmi. Reinson Wekesa. Kuna Zacharia Malenya? Utatoa maoni? Haya on Wekesa. Uanze kwa majina, you have less than a minute Sir.

**son Wekesa**: Kwa majina ni Reinson Wekesa Khaemba kutoka katika Machewa location, kijiji cha Lukhome, Lukosi Primary. kuwa kijana, nimesoma katika shule ya msingi kutoka katika darasa la kwanza mpaka darasa la nane. Lakini sijaweza ku----

**Maranga**: Please give him time to give his views.

**son:** Sasa kulingana na hayo, nimekosa kuoendelea na shule kwa ajili ya matatizo ya magonjwa, halafu na kuligana na hii ption. Kulingana na vile kutoka 1985 corruption zile zimekuwa hapa za kivita, kulingana na makabila mbali mbali. Tribalism. a hii Trans Nzoia vile mmesikia tuko na tribalism, makabila arubaini na mbili. Lakini kwa hayo katika Katiba hii mimi nikiwa kama a – youth mdogo pia hata nyumbani tumekosa kuwa na kimaendeleo.

**Maranga**: Pendekeza?

**son**: Sasa napendekeza ya kwamba, tunahitaji kwa ofisi ya finance watufikirie. Halafu watutumie kitu kidogo pia tufanye katika deleo. Na vile niko hapa hivi, niko na mama na baba lakini ni wakongwe sana na hawajiwezi.

**Maranga**: Sasa unataka wasaidiwe?

**son:** Sasa nahitaji wasaidiwe. Afya zao ni mbaya kwa ajili hata hawatibiwi. Na pia mimi mwenyewe nimekuwa mgonjwa kwa mrefu na hata nimekosa vile naweza kutibiwa na ningehitaji Katiba hii ya Serikali hii, pia hata mkinipa ruhusa na mjitoe na kwa gari, nkinipa gari niko tayari twende mpaka niwaonyeshe penye tunaishi. Ni katika sehemu ya mlima. Na wakati huyu Mzee amekuwa Bungoma Kimilili ni mzee ambaye amefanya kazi na Wahindi katika hii nchi ya Kenya. Na katika hii Africa nzima, we have 53

ries na katika hii Katiba ninawaombeni.

**Maranga**: Asante, na sisi tumechukua maoni yako, kwa ile njia umeongea na tumenasa sauti yako hapo. Asante nakuomba e sahihi. Okay, nataka kumpa mwingine nafasi. Next is Zacharia Malenya. Halafu tutapata Mendi Matende, ako? Uwe karibu a.

**aria Malenya**: Mimi ni Zacharia Malenya, mkaaji wa Kimilili division. Mara ya kwanza uchaguzi ujao ukaweze kuchaguliwa ia mashinani. Tuanze udiwani, twende ubunge halafu Presidential. Tusichanganye kwa sababu labda kunaweza kuwa na mengineo. o la pili, tukiangalia upande wa hizi sheria ambazo zimekuja mpya mfano ni miti. Sheria imetungwa kuwa unapokata miti, sijui uende ub-chief, uende kwa nani. Sheria hizo zinaatuumiza sana ingefaa ziondolewe.

de mwingine, tunaona kuwa upande wa budget. Mimi ningependekeza ile Wizara inayohusika ikaweze kufika katika wananchi ywe watoe maoni yao vile wanahitaji. Mwananchi aseme, kitu hiki kikifanywa bei fulani, inaweza kutusaidia sisi wananchi wa chini. usikia tu, kitu fulani kimeongezwa bila sisi tuoa maoni. Jambo la mwisho ni kuwa, katika nchi yetu tumeidhinisha Kiswahili lakini poona hotuba ambayo ni hotuba muhimu sana labda ni siri yetu sisi Wakenya, hotuba inatolewa kwa Kingereza yule mkongwe anganyikiwa. Kwa hivyo mimi napendekeza kuwa hotuba yoyote ama sheria iwekwe hotuba yoyote ya Serikali iweze kuhotubiwa Kiswahili ambayo ni lugha ya taifa, ambayo tunaijua.

**Maranga**: Asante kwa maoni yako, Netty Matende.

**Matende**: Asante sana kunipa nafasi hii. Mimi ni Netty Matenda, kutoka Lakamet farm hapa Saboti. Mimi napendekeza le wa upandaji wa miti. Upandaji wa miti nikiangalia vile natembea watu wadosi, wenye wako na mashamba kubwa, waruhusu kuingia kwa shamba yao kupanda miti. Na huyo mdosi ndio anakata miti kweli. Naomba Serikali iendelee kuhukumu watu wadosi, nde miti kwa sababu miti pia inaleta mbegu, kwa sababu mimi ndimi natembea na mbegu. Na pia mbegu watu wapande. Lakini watu hawapandi mbegu na miti inaendelea kupandwa na watu wanaendelea kukata miti na mimi ndio natembea na mbegu. ba Serikali inisaidie sana, kwa sababu PI inatoa mbegu. Na kumalizia naomba Serikali inisaidie sana kwa sababu natembea na u kuwapatia wakulima wapande. Asante sana mbarikiwe

**Maranga**: Asante, George Situma, hayuko. Do we have Cherotich Kapruko, ndiye huyo mama? Haya karibu. Huyo atafuatwa chael Odira. Ako? Hayuko. Do we have Annet Matata? Huyo hayuko, Alice Nyongesa. Hayuko. Martin Waduasi. They have y spoken. And Nancy Kiboi, student still? Okay. Then we have Mildren Sabwani? Do we have Stella Kapkana? Uko? Okay, e Margreti Kwalya? Utafuata huyo. Kuna Ernest Simiyu. Kunaye. Do we have Obicha Silvesters? Okay. Do we have Jimmy iri and Juma Moris? I think he spoke. Sasa tuanze na Cherotich Kaburuko.

na majina yako.

**otich Kaburuku:** Ani kokonyitaab cherotich Kaburuk.

**slator:** Yeye ni nyanya ya Cherotich Kaburuku.

**otich:** Abooye korooni, kikesikyo koroanitinyi, kiimech chumbek akooy ngy ba**.**

**slato**r: Yeye ni mtu wa nchi hii, alizaliwa hapa na wazungu walimsumbua**,** mpaka wakaenda.

**otich**: Mebere mi kooret nyikikekonech

**slator**: Na hakuna nchi waliwapea.

**otich**: Kikwa biikoab emoonik alk, serekali nyi kinyaare

**slator**: Kila kabila wakaingia hapa Serikali ndio waliharibu

**otich**: Kiyeeu mono, kiketyi biko mberenik kwa, kuwunda buch

**slator**: Hawakurudi kupeana mashamba kwa wale watu walikuwa wenye mashamba, wakawawacha tu bure.

**otich**: Konem chembek tuukyo, kengotu buch

**slator**: Wazungu wakawanyang'anya ng'ombe wao na wakaenda wakabaki bure.

**otich**: Nde oyyini kumwoech kyaal koreet nyiki nyenyo, nyiki meyeme kyaal.

**slator**: Na juzi wakawambia sasa mnanunua nchi yenu na haikuwa nchi ya kuwauzia.

**otich**:Kikoyto mberenik aab kitalale, kyboyiit bikaab sang'

**slator**: Wakapeana Kitalale Scheme ikawa ya wale watu wa kutoka nje.

**otich**: Chikimiteyu kunyoar mono kiy

**slator**: Na wenye walikuwa hapa wakabaki tu hivyo.

**otich**: Kenyenyacheek wooktaab kiborowo, nengyi mi kokochine serikali biiko chi kimetinye.

**slator**: Forest ya Kiboroi ilikuwa ni yao na sasa Serikali tena iko inawapa wale ambao hawakuwa nayo.

**Maranga:** Muulize anapendekeza nini?

**otich**: Kiuune kirigete kule nyenyo koret

**slator**: Anasema tukae tukijua nchi ni yetu

**otich**: Kuttok komositinyi kule nyenyaachek, mebere bo biiko tukul.

**slato**r: Sehemu hii ijulikane ni yetu na isiwe ni ya watu wote.

**otich:** Kisokitye acheek sang, nde bikaab sang kukwa angu tambas.

**slator**: Ati sasa tunaumia nje na wale wenye kutoka nje wakaja wakafaidika.

**otich:** Chaang chimetinye mbereniik kunyitinyi.

**slator:** Wengi ndio wenye hawana mashamba saa hizi.

**otich:** Kemeche serikali kuketwech koreenyo.

**slato**r: Tunataka Serikali itupatie nchi yetu.

**otich:** Ndo mbereniikyoo.

**slator:** Au mashamba yetu

**otich:** Nde sikikochi biiko alaak tukul mberenik, ndeacheek bikaab korret kewuye ne?

**slator:** Na kwa nini watu wengine wote walipewa schemes na sisi Wasaboti tuko namna gani?

**otich:** Kekureneech acheek bikaab koony.

**slator**: Sisi tunaitwa Wakonyi Elgon Masaai.

**otich:** Kemeche mbono ngaleek cho tese serekali kumwoweech

**slator:** Hatutaki maneno ile Serikali inaendelea kutuambia.

**otich:** Serikaliit nye kiwulyo bikoo kiyey boriet

**slator:** Serikali ndio iligonganisha watu mpaka wakapigana.

**otich:** Ng'etye wohin kukwooni woli, Nge'tye woolin, kukwooni

**slator:** Wakitoka huko wakikuja hapa,wakitoka huko wakikuja hapa na serikali inaona tu na kunyamaza.

**Maranga**: Ya mwisho mama?

**otich:** Kung'alaal serekaliit nyi toboon sikibuur nyi karaam.

**slator:** Serikali iongee mambo mazuri ndio sisi tukae vizuri.

**Maranga**: Mchukue aweke sahihi. Anayefuata ni Kapkara. Wapi yeye? Sijui unaitwa Tela? Wewe ni Tela kabisa. Tela ara then we have Margret Kwalya, and then Ernest Simiyu halafu nitapata yule Mzee anaitwa Obicha.

**Kapkara**: Mimi ni Tela Kapkara.

**Maranga**: Toa mapendekezo Mzee.

Wacha nisimame, wakati wa mwaka wa thelathini na mbili ndio walihamisha sisi kupeleka Uganda. Na kufika huko Uganda, ka wa arubaini na mbili, wakaramojong' walinyang'anya sisi ng'ombe na kuua watu. Tulitoroka huko tukaenda Tanzania, tukapata nia Kenya ikawa mbaya kwa sisi Wakenya. Tukarudi, na mimi nasema nchi ya mtu mwingine ni mbaya kabisa. Si nzuri. Mimi na wakati wazungu walikwenda, kwa nini wale watu walifanyia wazungu kazi mbona wao hawakuweza kurudi kwao? Sisi hatuko a Turkana. Sisi hatuko nchi ya West Pokot, sisi hatuko nchi ya Waluhya. Sisi hatuko nchi ya Kikuyu na nchi yetu ilikuwaje halafu makabila yote walikuja na sisi tunatangatanga mpaka saa hii.

ndekezo mimi nataka Majimbo. Nataka chifu, sub-chifu na mukasa ndio wapee watu makao. Ya mwisho wale matajiri wa heka bili, elfu tatu, wapeane heka mia moja.

**Maranga**: Thank you Mzee.

Halafu yale mashamba yamepewa masikini yawekwe ng'ombe. Mbona wakati wa Kenyatta, ilikuwa Kenyatta anampa mtu ba na ng'ombe. Ng'ombe walienda wapi? Mimi nataka namna hiyo.

**Maranga:** Asante, weka sahihi hapo na utupe memorandum yako. Mimi naona wewe ni Tela kabisa. Tupate Margret Kwalyia.

**gret Kwalyia**: Mimi jina langu ni Margret Chelang'at Kwalyia ni mkaaji wa hapa Saboti upande wa Sikwa na mimi tambulisha kama ni mama mkunga. Nimeshukuru sana ninapoona hivi vichwa vyote nafikiri mmepitia kwa mikono yangu. Ingawaje wa nafikiri alipitia kwa mama mkunga ndio akamsaidia akazaliwa. Asante sana, jambo ambalo ningependekeza ni kwamba kama mkunga sina makao, nimeenda kuishi msitu na ninawasaidia wengine kule. Nafikiria wangefurahia niwe karibu nao kwa vile idiana na Saboti Health Centre hapa. Sasa wananitafuta mimi mpaka msituni kule na unajua madaktari wetu bado wangali wadogo elewi kupapasa tumbo vile sisi tunajua inakaa namna gani.

**Maranga**: Wewe ni dakitari wa kienyeji?

**gret:** Mkunga.

**Maranga**: Okay, kwa hivyo ungetaka msaidiwe na Serikali, nyinyi kama wakunga?

**gret**: Mimi ningependa hivyo, kwa sababu raia hawawezi unaweza kumkuta mtu hajiwezi na nimemsaidia, hata korokoro moja hata kilo ya sukari hana, lakini tunamsaidia kwa huruma yangu. Lakini anapokwenda hospitali anateseka njiani lakini kama ningekuwa ningemsaidia kwa sababu niko na moyo wa huruma ya kumsaidia.

**Maranga**: Asante mama.

**gret:** Mimi sina mengi ya kuongea ijapokuwa nataka raia wangu waendelea kuwapatia watoto birth certificate ili wapate kuendelea somo.

**Maranga**: Asante mama, thank you very much na endelea na kazi yako nzuri. Ernest Simiyu?

**st Simiyu**: Kwa majina naitwa Ernest mwana wa Simiyu kutoka Kisawai location. Maoni yangu ya kwanza, magari mabovu arani wenye kuyamiliki washtakiwe badala ya wenye kuendesha. Ya pili matajiri wa mashamba makubwa ambao wana wafanyi a wamefanya kazi zaidi ya miaka kumi na kuendelea mbele, wapewe sehemu ya shamba kidogo badala ya kuyauza mashamba na wacha wapweke.

wisho ni ushuru wa Serikali, taxes, ugawanywe ingawanywe kwa viwango mbali mbali kulingana na uwezo wa Kenya. Ikiwa ia kumi na nane ni ya wale wa juu, asilimia mbili iwe ya wale masikini. Asante.

**Maranga**: Mzee Mbunyi, nani huyu?

**na**: Obicha Silverious

**Maranga**: Obicha I did not know that you are here, proceed.

**na**: Pendekezo langu la kwanza linahusu Wabunge maalum. Tangu tupate uhuru, Rais amekuwa anachagua Wabunge kumi na mbili m na wote wamechaguliwa muda huo wote sijaona wakiwa na kazi maalum vile maana ya maalum katika kamusi.

**Maranga**: What do you recommend?

**na**: Hii Katiba mpya ipee Bunge uwezo wa kuteua Wabunge maalum, sio vyama. Na wateuliwe kama lifuatalo ikiwezekana: a, wapewe nafasi mbili Bungeni. Age between 18-30 years. Elimu wakuwe na sound education nikimaanisha at least a graduate a recognized university. Akina mama ambao ni wengi katika nchi hii wamesahaulika, wapewe nafasi tatu. Hao wote umri wao emee kila binafsi na wawe na elimu kufika university. Wenye wana kasoro mwilini, walemavu, sio pendekezo lao, ni Mungu aliumba vakuwe na wawakilishi wawili katika Bunge letu ili watetee hao. Hao wote lazima wakuwe na elimu ya kutosha kama university.

**Maranga**: Ya mwisho.

**na**: Watu wa LSK wakuwe na mtu mmoja, COTU, mtu mmoja na Human Rights mtu mmoja. Wote watu kumi na wawili wawe Bunge letu.

**Maranga**: Thank you very much. Mzee start with your full names.

**ed Nyonyi**: I am Wilfred Ngonyi from Kiminini. Masomo iwe free na Serikali igharamie mambo yote ya shule. Umasikini gilia watu na magonjwa yameuwa watu wengi shauri ya kitu wanaita cost sharing. Tungetaka medical services, kwa district tals na clinics ziwe free. Wananchi watibiwe bila kuulizwa pesa, na Serikali igharamie mambo ya mishahara ya daktari na madawa.

ncial administration, tumeangalia tumeona hakuna kazi nzuri wanafanya. Tungetaka provincial administration, PC, DC na DO ve mbali tubakie na chifu. Lakini muongozo wa district uongozwe na county council. Kwa province watu wachaguliwe au kamati liwe kutoka kila district moja moja wafanye provincial committee ile itazungumza mambo ile PC alikuwa anafanya.Tungetaka tena

warudi misituni, ile ilikuwa ya Serikali, walime huko na wapande miti vile walikuwa wanapanda zamani ndio miti irudi kiwango . Yangu ni hayo tu.

**Maranga**: Asante Mzee Ngunyi na kwa niaba ya Tume ya Kurekebisha Katiba nataka kusema sasa tumefika mwisho wa kikao hapa upande wa Saboti, na kwa hivyo mimi nashukuru sana watu wa Saboti, lakini kabla sijamaliza hebu niulize mwenzangu Dr. nissioner Mosonik kama ana la kusema.

**Dr. Mosonik**: Sina chochote ila kuwaeleza tumefurahia maoni yenu, mmesema watu wengi zaidi, umati umekuwa hata wa nda sehemu zingine. Tumeyasikia kwa makini, tumeyaandika, tumeyanasa kwa kitambo na tutayapeleka kwa Tume. Asanteni sana.

**Maranga**: Basi mimi vile nilikuwa mwenyekiti wa kikao hiki, mimi ningesema asante kwa niaba ya Tume ya Kurekebisha Katiba. i yenu yatachukuliwa kwa ile hali mmeyatoa leo na mimi sijawahi kuona umati mkubwa vile tumeona hapa leo, hii ni shukrani kubwa onyesha mna hamu sana ya kuona Katiba ambayo italinda nchi katika miaka mingi ijayo. Kwa hivyo maoni yote mmetoa sisi angalia tu. Tutayapima ili tuweze kujua inafanyika namna gani. Basi kwa hayo nasema asanteni na naomba tupate maoni ya mwisho aweze kuondoka. Asanteni, na Mungu awabariki.

**na Khaoya**: Kabla ya kufunga sisi tuko na furaha kubwa leo. Mimi ambaye nimejishughulisha kupanga hapa kazi hii, tumeweka tipiki na vikaratasi wamezunguka skuli zote, ningekuwa nastaajabu kama hamngekuta watu. Kwa hivyo sisi tunashukuru vile umilia mpaka jioni hamjakula lunch tunaonelea hata kidogo wakati mnamaliza mtafuatana na Bwana Ngunyi, hata kama ni maji tu kwamba mnatoka kwa Saboti, ndio nyumbani kwa Mzee Khaoya, hapa mmepita mlima ambapo kuna murram, hapo ndio kwangu. ukuru sana na pengine tungemaliza na sala.

**ta Cheripadoi**: Wacha tuiname wote na tuombe. Mungu baba, Mungu wa ajabu, tunakurudishia asante kwa kutuongoza hadi i huu Jehova. Naona ni wakati mzuri Bwana tumesema ni asante. Waliohudhuria wote tunawakabidhi mikononi mwako. Wageni wanaoondoka Bwana nawakabidhi mikononi mwako. Wanapoenda na magari yanayoendeshwa na watu uwabariki na uwatunze a. Na wakati mwingine tuonane wote tukiwa wazima tutasema ni asante. Jehova lenye sijagusia upate kugusia. Naomba machache nini katika jina la Bwana.

ng closed at 5.00 pm